# Nipashe

Jumanne Desemba 8, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580423

www.ippmedia.com

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




UKURASA 11

**MWANAFUNZI** kidato cha 2 akutwa chumbani ameuawa



UKURASA 2

**UKATILI** wa kutelekeza familia washamiri

UKURASA 3

# Maagizo manne ya serikali bei ya saruji

## **PM** akutana na wadau, wazalishaji, viongozi wa serikali na kueleekeza...*Endelea Uk. 3*



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza katika kikao kwa njia ya mtandao na Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Kaimu Katibu Mkuu - Uchukuzi, Wakuu wa Mikoa, Maofisa Biashara wa Mikoa, Mawakala wa Saruji mikoani na Wakurugenzi wa Viwanda vya Saruji. Aliongoza kikao hicho akiwa ofisini kwake, Mlimwa jijini Dodoma. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

## YALIYOMO

UKURASA WA 16

**MAMIA WAKOSA MAKAZI KISA NYUMBA KUEZULIWA**

ZAIDI ya kaya 108 za vijiji vitatu vya Kata ya Ipinda katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, hazina mahali pa kuishi baada ya nyumba zao...

# Maoni mchanganyiko Maalim Seif kujumuishwa serikalini

UKURASA 2

## Bunge na CHADEMA wakinzana wabunge wa Viti Maalum

UKURASA 2

**MICHEZO** RUVU SHOOTING YATAJA 'USALITI' KIPIGO YANGA UK. 23

MAONI, KATUNI UK. 6

# Mwanafunzi akutwa ameuawa chumbani

**Na Rose Jacob, MWANZA**

MWANAFUNZI wa kidato cha pili katika Shule ya Sekondari Katunguru, aliyefahamika kwa jina la Vincent Renatusi, amekutwa ameuawa chumbani kwake jijini Mwanza alipokuwa anaishi, huku mwili wake ukiwa na majeraha shingoni.

Kwa mjibu wa Kamanda wa Polisi mkoani Mwanza, Murilo Jumanne, mwanafunzi huyo mwenye umri wa miaka 17, mkazi wa Mtaa wa Msumbiji Kata ya Kawekamo wilayani Ilemela mkoani Mwanza, aliuawa na vitu vyake kuporwa.

Kufuatia tukio hilo la mauaji, Jeshi la Polisi mkoani hapa linamshikilia mtu mmoja, Hamisi Omary, mwenye umri wa miaka 19 mkazi wa Nyasaka Msumbiji, kwa tuhuma za kutenda kitendo hicho.

Kamanda Murilo alidai kuwa mtuhumiwa huyo alikiri kufanya mauaji hayo baada ya kuhojiwa.

"Tunamshikilia Hamisi Omary kwa tuhuma za kumuua mwanafunzi Vincent Desemba Mosi majira ya saa 11:00 asubuhi," alisema Kamanda Murilo na kuongeza:

"Ametupeleka sehemu alipokuwa ameuza vitu alivyokuwa amepora chumbani kwa marehemu, na aliyevinunua vitu hivyo naye tumemkamata."

Aidha, Kamanda Murilo alisema vitu mbalimbali vilivyoporwa ni runinga, redio aina ya Sub woofer, ambavyo vinadaiwa kuuzwa kwa Erasto Jackson, mkazi wa Kitangiri.

Mtuhumiwa huyo naye anahojiwa kwa tuhuma za kupokea mali za wizi.

# Wachambuzi waunga mkono uamuzi wa ACT-Wazalendo

**Na Beatrice Shayo**

WACHAMBUZI wa masuala ya siasa na wasomi wametoa maoni yao kuhusu uamuzi wa Chama cha ACT-Wazalendo kuridhia kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK), kuwa ni kitendo cha busara.

Hata hivyo, baadhi ya watoa maoni hayo walidai chama kukosa msimamo baada ya awali kupinga matokeo ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu.

Wachambuzi wengine wametafsiri kuwa ACT-Wazalendo wameangalia maslahi mapana ya Wazanzibari.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti walisema, kitendo cha chama hicho kuridhia kuingia katika SUK ni cha busara na kutasaidia chama kuendelea kujijenga vizuri.

Profesa wa Chuo Kikuu cha Ruaha (Ruco), Gaudence Mpangala, alisema uamuzi wa Maalim Seif ni wa busara ingawa mwanzo walipinga matokeo.

Alisema siasa za Zanzibar anazifahamu. "Kwa kuangalia siasa za Zanzibar, ametumia busara namuunga mkono katika hilo," alisema.

Profesa Mpangala alisema kuwapo kwa SUK kumesaidia kupunguza msuguano wa kisiasa visiwani humo.

Alisema awali kulikuwa na msuguano mkali baini ya Chama cha Wananchi (CUF) na Chama Cha Mapinduzi (CCM) na vilikuwa vikisuluhishwa mara kwa mara.

"Msuguano ulikuwa siyo mzuri, ilikuwa hakuna kuzikana, kusaidiana kwa sababu ya kisiasa, endapo Maalim Seif angekataa ingesababisha mvutano," alisema.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Richard Mbunda, alisema Maalim Seif ni mtu mwenye uzoefu wa siasa za kuzira, na kitendo chake cha kukubali ni cha busara.

Alisema wanapokuwa wanazira jambo fulani wanajinyima fursa kitendo ambacho alikuwa akikifanya Maalim Seif katika serikali ya awamu ya saba.

Mbunda alisema wanapokubali kuingia kwenye Serikali ya Umoja ya Kitaifa kunawapa fursa ya kuwapo kwa wizara na inakuwa rahisi kuziwasilisha hoja zao kuliko kususia ambako kunawaletea madhara.

Kwa mujibu wa mhadhiri huyo, uamuzi wa ACT- Wazalendo ni moja ya kubadili mbinu kwa kuwa wameona mbinu za zamani hazijawapa tija.

"Siasa za kususia hazina tija, unatakiwa kufanya siasa za kugusa hisia za watu wengi. ACT-Wazalendo kinahitaji kukua na wameona ni bora kuingia katika serikali ya SUK," alibainisha.

Aliyewahi kuwa Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Profesa Abdallah Safari, alisema ubinafsi umesababisha usaliti bila kujali walioumizwa kwenye uchaguzi mkuu ambao waliupinga.

Alisema huu ni wakati wa CHADEMA kufanya vizuri wasikubali kubadilika kwa kuwa wana mtaji mzuri wa wanachama.

ACT -Wazalendo kilifikia makubaliano ya kuingia katika SUK baada ya kikao cha Kamati Kuu ya chama hicho kilichofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, ambacho pamoja na mambo mengine kilitoa masharti kikitaka watu wote waliohusika na matukio ya uvunjifu wa haki za binadamu wakati wa uchaguzi mkuu wachukuliwe hatua za kisheria, ili kupunguza majeraha kwa wananchi na kuhakikisha chaguzi zijazo zinakuwa huru na haki.

Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, alisema Kamati Kuu ilizingatia hali ilivyo Zanzibar hivi sasa na siasa za chuki na uhasama kurudi upya kutokana na makovu yanayotokana na uchaguzi wa mwaka huu.

Novemba 19, mwaka huu, wakati akitangaza Baraza la Mawaziri, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, alisema walikiandikia barua chama hicho kwa ajili ya kupeleka jina la Makamu wa Kwanza wa Rais.

Alisema pia alilazimika kuacha nafasi mbili za mawaziri wa Afya na Biashara kwa ajili ya chama hicho endapo kingeridhia kuingia katika SUK.

Maridhiano yaliyofanywa mwaka 2010 ndiyo yaliwezesha kuwapo kwa mabadiliko ya Katiba ya Zanzibar na chama kinachopata kura zaidi ya asilimia 10 kinaruhusiwa kuingia katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, mwaka huu, ACT- Wazalendo kilipata kura zaidi ya asilimia 10, hata hivyo, awali kilipinga kuingia SUK kwa madai kuwa uchaguzi haukuwa huru na haki.

Katika mkutano wa pamoja baina ya ACT-Wazalendo na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), viongozi wa vyama hivyo walikaririwa wakisema kuwa hakukuwa na uchaguzi bali kulikuwa na uchafuzi.

**MAALIM KUAPISHWA LEO**

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Ikulu Zanzibar, Maalim Seif ataapishwa leo kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais katika viwanja vya Ikulu visiwani humo.

Pia, jana mchana Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliwateua Naibu Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Nassor Ahmed Mazrui na Mwanasheria wa ACT-Wazalendo Zanzibar, Omar Said Shaaban, kuwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.



Mbunge wa Nachingwea mkoani Lindi, Dk. Amandus Chinguile (mwenye suti), akimjulia hali mgonjwa Juma Seif, alipotembelea hospitali ya wilaya juzi, kuzungumza na watumishi ili kujua kero zinazowakabili. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bunge, CHADEMA wakinzana wabunge wa Viti Maalum

**Na Mwandishi Wetu**

BUNGE na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) wametoa kauli zinazokinzana kuhusiana na suala la kuvuliwa uanachama wabunge wa Viti Maalum kwa tiketi ya chama hicho.

Bunge limesema halijapokea barua ya CHADEMA, kuhusu uamuzi wa Kamati Kuu ya chama hicho iliyokutana kwa dharura kuwajadili wabunge wa Viti Maalum 19.

Jana Nipashe ilipokea taarifa kuwa CHADEMA imeshawalisha barua ya uamuzi wa Kamati Kuu kwenye muhimili huo wa kutunga sheria na kuisimamia serikali.

Alipoulizwa kuhusu kama Bunge limepokea barua kutoka CHADEMA, Katibu wa Bunge, Stephen Kagaigai alisema: "Waulize wenyewe."

Alipoambiwa tayari wameulizwa na wamekiri kuwasilisha barua, alisema: "sijaiona."

Taarifa zilizothibitishwa na CHADEMA zilisema: "Bunge lilishapelekewa barua tangu mwezi jana. Baada tu ya uamuzi."

Novemba 27, mwaka huu, CHADEMA ilitangaza kuwavua nyadhifa zote aliyekuwa Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake la (BAWACHA), Halima Mdee, na viongozi wengine, pamoja na kuwafuta uanachama.

Aidha, Mdee na wenzake 18 walisema watakata rufani Baraza Kuu kupinga uamuzi huo, na kwamba wataendelea kuwa wanachama wa hiari.

Wabunge hao waliapishwa Novemba 23, mwaka huu, na wakati akizungumza kwa niaba ya wenzake, Mdee alieleza kuwa wana baraka za chama hicho, jambo ambalo lilipingwa vikali na Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe na Katibu Mkuu, John Mnyika.

Viongozi hao walisema fomu za kupeleeka majina Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuhusu viti maalum hazikujazwa na Katibu Mkuu kwa mujibu wa utaratibu.

HABARI KITAIFA

# Tisa jela miaka 30 kwa ubakaji

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

WATU tisa wilayani Kishapu mkoani Shinyanga, wamehukumiwa kwenda jela miaka 30 kwa makosa ya ubakaji wa watoto kuanzia Januari hadi Novemba, mwaka huu.

Matukio 91 yaliyoripotiwa kesi 43 bado zinaendelea mahakamani.

Mkuu wa Dawati la Jinsia na Watoto kutoka Jeshi la Polisi wilayani Kishapu, mkoani Shinyanga, Rose Mbwambo, alisema hayo juzi wakati wa maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia wilayani, ambayo kilele chake ni Desemba 10, mwaka huu.

"Dawati la jinsia bado tunakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa mashahidi kwenye kesi hizi za ubakaji dhidi ya watoto, na ndiyo maana hukumu zake zinachukua muda mrefu, sababu ya jamii kuogopa lawama na uhasama wa kifamilia," alisema Mbwambo.

Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Nyabaganga Taraba, alisema matatizo ya kubakwa kwa watoto wa kike yanatokana na imani za kishirikina na kuitaka jamii iachane na vitendo hivyo ambavyo vina kiuka haki na utu wa mtoto.

Alisema serikali wilayani humo itaendelea kuwachukulia hatua kali wananchi wote wanaendekeza masuala ya ukatili wa kijinsia, huku akiyataka mashirika na watendaji wa serikali kuendelea kutoa elimu ya ukatili ndani ya jamii pamoja na madhara yake.

# Serikali yaagiza mambo 4 bei ya saruji

**Na Edwin Mhagama**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ametoa maagizo manne kwa wadau wa saruji na viongozi wa serikali katika kudhibiti bei ya saruji pamoja na upatikanaji wake nchini.

Waziri Mkuu alitoa maagizo hayo jana, jijini Dodoma, katika mkutano kwa njia ya mtandao na wadau wa saruji wakiongozwa na wawakilishi wa kampuni za saruji, wakuu wa mikoa na watumishi wa Wizara ya Viwanda na ya Uchukuzi, ambapo aliwaagiza viongozi wa serikali kutembelea mara kwa mara viwanda vya saruji.

"Viongozi wa Wizara ya Viwanda endeleeni kutembelea viwanda na kusikiliza matatizo, wana ushauri wa kuzungumza na serikali, pamoja ya kwamba tumewahamasisha kuwekeza nchini, lakini kuna umuhimu wa kuwatembelea tukasikie matatizo yao... hao ndiyo mabalozi wa kuita wawekezaji wengine," alisema Majaliwa.

Waziri Mkuu alizitaka kampuni za uzalishaji wa saruji kuhakikisha zinaongeza wigo wa usambaji na uzalishaji nchini kwa kuhakikisha mawakala wa usambazaji saruji wanaongezeka mpaka maeneo ya vijijini, ili kuleta unafuu kwa wananchi na kuhakikisha saruji inapatikana.

"Kampuni za saruji tanueni wigo wa mawakala, kuwe na mawakala angalau kila mkoa kwa kila kampumi, ili bidhaa zenu ziweze kufika kwa mawakala hao kwenye mikoa ili saruji ipatikane mpaka vijijini," alisema Waziri Mkuu na kuongeza:

"Kwa hiyo ongezeni mawakala ili saruji iweze kufika kwa wakati kwa wananchi."

Katika agizo lingine, Majaliwa liitaka Tume ya Ushindani kuhakikisha bei ya saruji inashuka na kuwa yenye tija kwa wananchi kulingana na gharama.

"Tume ya ushindani mnatakiwa kujua kama bei ya saruji ni shindani na yenye tija kwa wananchi wetu, hili ni jukumu lenu kupita kuona kama bei zinazotumika ni bei halisi... bei imekuwa kubwa sana, na inatuletea mgongano kati ya wananchi na serikali," alieleza Waziri Mkuu.

**AKATAA BODI YA SARUJI**

Katika hatua nyingine, Majaliwa alisema kwamba hakuna ulazima wa kuunda Bodi ya Saruji, na kuwa ni bora kuanza kushughulikia changamoto zilizopo kwanza, ili kuepuka gharama.

Kadhalika, aliwataka wakuu wa mikoa kuhakikisha wanakuwa wanafanya ziara katika viwanda vya saruji katika mikoa yao.

Kwa upande wao, wawakilishi wa kampuni za uzalishaji saruji walisema wanajitahidi kupunguza gharama za bidhaa hiyo licha ya kwamba wanakabiliwa na vikwazo mbalimbali vikiwamo ukarabati wa mashine za viwanda, umeme pamoja na gharama za usafirishaji.



Meneja bidhaa wa kampuni ya Tigo, Mkumbo Myonga, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, wakati wa kuzindua kampeni ya kufunga mwaka, wateja watapata fursa ya kujishindia pikipiki au televisheni za kisasa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ukatili wa kutelekeza familia washamiri Njombe

**Na Elizabeth Kilindi,** NJOMBE

MATUKIO 43 ya ukatili wa kutelekeza watoto Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, yameripotiwa kwa kipindi cha mwezi Julai 2019 hadi Septemba 2020.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, Ofisa Ustawi wa Jamii wa halmashauri hiyo, Averino Chaula, alisema matukio hayo ni yaliyoshindikana kwa ngazi za awali.

"Inawezekana kuna matukio mengi kwa sababu haya ni yale ambayo yameshindikana hatua ya awali, yaani ngazi ya jamii yameshindikana, wakipeleka ngazi ya kata yamewashinda kwa hali hii inaweza ikakupa picha," alisema Chaula.

Katika kuelekea maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia, Chaula alisema wanaume wengi wanaotelekeza familia wamejijengea mazoea kwamba mwanamke ndiye anapaswa kutafuta kipato.

"Ukizungumza nao walio wengi tayari wana mazoea, watu wengi wa mkoa wa Njombe mama ndiye mtafutaji, baba anachohakikisha anamtafutia shamba mama, watoto wamekulaje, wamevaaje hawajali, wanamuachia mwanamke na mwanamke mzigo unapokuwa mkubwa wanakuja kukimbilia," alisema.

"Wapo wengine kwa sababu ya ndoa za mitala unakuta baba amekimbilia upande mmoja amesahau upande mwingine, kwa hiyo watoto wa upande wa pili wanakuwa waathirika wa ndoa mpya matukio mengi yanafanana, hivyo pia kuna watoto wa nje ya ndoa baba amezaa bila ya kuoa akishazaa huko wanalea kwa siri, lakini mwanaume anapokosa kuwajibika mambo yanakuja hadharani," alisema Chaula.

Aliwataka wanawake kuepuka kuweka mahusiano ya siri na mwanamume ambayo baadaye yatasababisha kutelekezewa watoto.

"Ukishapata mchumba mkishaanza mahusiano hujui malengo yake umkatae kama unaona anaeleweka nenda tu kwa wazazi, ili hata mtoto anapozaliwa baba awajibike asiwe na sababu za kukwepa," alisema.

Alitoa wito kuwa jukumu la kuzuia ukatili kwa watoto na wanawake ni la kila mtu hivyo jamii isisite kufichua vitendo hivyo.

HABARI KITAIFA

## Ndugai awaambia wahitimu watumie taaluma kujiajiri

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amewataka wahitimu wa Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA), kuacha kulalamikia serikali ukosefu wa ajira, badala yake watumie taaluma waliyoipata, kujiajiri na kupaisha uchumi wa kati nchini.

Amekipongeza chuo hicho kufungua tawi lao mkoani Dodoma, litakalowezesha wabunge kupata elimu ya uongozi, utawala na usimamizi wa fedha.

Akizungumza jana jijini Arusha wakati akiwatunuku vyeti wahitimu 1,952 wa ngazi ya Uzamili, Shahada, Stashahada na Astashahada za masuala mbalimbali ya fedha na TEHAMA, Ndugai aliwataka wahitimu kuachana na mawazo ya kikoloni ya kusubiri ajira za serikali na mashirika binafsi.

"Ninyi ni wataalamu wa masuala ya fedha mnajua jinsi ya kuzitafuta, kuwekeza na kuzipangilia, hivyo ondokeni kwenye mawazo potofu ya kusubiri ajira, wakati mmekalia utajiri nendeni mkajiajiri, nendeni mkawe chachu ya taifa, sababu nyinyi ni mabilionea wa nchi hii," alisema.

Ndugai aliwataka kuacha kutumia muda mwingi kwenye mitandao ya kijamii kurusha lawama na matusi kwa serikali na baadhi ya wazazi kutokana na kukosa ajira kwa kuwa haitawasaidia.

"Inakera sana kuona mhitimu wa chuo kikuu anatumia muda wake kutukana serikali na kuilaumu, badala ya kutafuta utajiri, kitendo hiki kinawafanya wapitwe kiuchumi na kimaendeleo na watoto wa darasa la saba ambao wengi hutumia muda wao, kusaidia wazazi shughuli mbalimbali za kiuchumi na baadhi hata kuanzisha miradi mikubwa," alisema.

Alitoa mfano wa mfanyabiashara ambaye ni marehemu bilionea Faustine Mrema, alisema hakusoma Chuo Kikuu, lakini ameacha alama ya miradi mikubwa ya hoteli ya Impala, Naura na Ngurdoto.

"Igeni mfano wake kama angetumia muda wake vibaya, leo tusingemkumbuka hapa licha ya kuwa ametangulia mbele ya haki badilikeni," alisisitiza.

Aliwataka kuacha kuchagua kazi na kujifungia mlango wa ajira kwa kutaka wawe wahasibu pekee wakati wana elimu ya kufanya kazi yoyote kwa kutumia utaalamu wao wa fedha na kuwa matajiri.

Alipongeza pia chuo hicho kuanzisha kozi mpya za Shahada za Uzamivu (PHD) na kuwapa wanafunzi mazingira bora na tulivu ya kujisomea ya Ngurdoto ambayo yatavutia wanafunzi wa mataifa mbalimbali, kuja kusoma na viongozi wa serikalini.

Kwa upande wake, Mkuu wa Chuo cha Uhasibu Arusha, Prof. Eliaman Sedoyeka, alisema chuo hicho ni bora barani Afrika na wanajipanga kuanzisha kozi za Shahada za Uzamivu hivi karibuni.

Kuhusu kuhamishia wanafunzi kwenye hoteli ya nyota tano ya Ngurdoto Mountain Lodge, alisema baada ya kuona sekta ya utalii imeathirika na janga la corona na kwa kuwa wao ni wabobezi na wasimamizi wa masuala ya fedha na biashara, waliona vyema kupeleka wanafunzi hapo ili kuinua uchumi na biashara hiyo.




Mhandisi wa Mitambo ya Mawasiliano, Uongozaji na Ufuatiliaji wa Mienendo ya Ndege wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), Ednah Mbwana, akitoa elimu juu ya shughuli zinazofanywa na kitengo hicho, katika banda la TCAA kwenye maonyesho ya 5 ya bidhaa za viwandani yanayofanyika katika viwanja vya Sabasaba, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

# TAKUKURU yaokoa mamilioni zaidi ya walimu mikopo umiza

**Na Mwandishi Wetu**, TABORA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Tabora, imefanikiwa kurejesha zaidi ya shilingi milioni 17, ambazo walimu wanne na mtu mwingine walidhulumiwa na wakopeshaji wasio na vibali pamoja na mfanyabiashara.

Hayo yalibainishwa jana na Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Tabora, Mussa Chaulo, wakati wa mkutano na waandishi wa habari.

Alisema katika tukio la kwanza, TAKUKURU ilimrejeshea Mwalimu Veronica Joseph shilingi milioni 6 kati ya 10 ambazo alikuwa akimdai mfanyabiashara Yusufu Kitumbo.

Alisema hatua hiyo ilifikiwa baada ya Kitumbo kushindwa kumpa gari alikuwa amekubali kumuuzia Mwalimu Veronica kwa kiasi cha shilingi miloni 10.

Alisema licha ya mwalimu kumaliza malipo baadaye alimdanganya na kulichukua gari kwa madai kuwa kuna mtumishi wake alikuwa anampa sehemu ya fedha za mwalimu huyo.

Chaulo alisema licha ya mwalimu huyo kudai kupatiwa gari alilolipia, Kitumbo alimzungusha na ndipo TAKUKURU iliingia kati na kufanikiwa kupata kiasi hicho.

Akizungumza baada ya kupata fedha hizo, Mwalimu Veronica aliishukuru Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tabora kwa kushirikiana na TAKUKURU kwa kufanikiwa kurejesha kiasi hicho, na kuwaomba waendelee kumbana ili aweze kumalizia kiasi kilichobaki cha shilingi milioni 4.

Katika tukio la pili, Chaulo alisema TAKUKURU imefanikiwa kuwabana Kampuni ya Misana Michael Mtaturu, Marco Maduka, na Dotto inazokopesha mikopo kinyume cha sheria na taratibu na kurejesha na kuokoa kiasi cha shilingi milioni 9.5 zilizokuwa na walimu watatu.

Alisema fedha hizo ni mali za walimu Sophia Mathew, Anna Mtaturu na Regina Mponeja.

Mkuu huyo wa TAKUKURU Mkoa wa Tabora alisema wamefanikiwa kurejesha kiasi cha shilingi milioni 1.5 kwa Boniface Daniel ambaye alikuwa kibarua wa Kampuni ya Simu ya Mkononi Tanzania(TTCL) baada ya kutolipwa haki yake na mtumishi wa TTCL.

Wakati huo huo TAKUKURU Mkoa wa Tabora kwa kushirikiana na Ofisi Mashtaka wa Serikali, inatarajia kumfikisha mahakamani mfanyakazi wa Manispaa ya Tabora, Sylvester Michael, kwa tuhuma za kujihusisha na vitendo vya rushwa, matumizi mabaya ya mamlaka na ufujaji na ubadhirifu.

Alisema kati ya Machi 2018 hadi Juni 2019, alikuwa amekusanya shilingi milioni 19.6, lakini kiasi cha shilingi 5.3 kati ya hizo hazikuwasilishwa benki.

# EPZA yahamasisha ununuzi bidhaa za ndani

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Uwekezaji wa maeneo maalum kwa ajili ya mauzo nje ya nchi (EPZA), imetoa wito kwa wananchi kununua na kutumia bidhaa zinazozalishwa na viwanda nchini kwa kuwa zina ubora wa hali ya juu kuliko zinazoagizwa nje ya nchi.

Mkurugenzi wa Uhamasishaji Uwekezaji wa EPZA, James Maziku, alisema hayo alipokuwa anazungumzia maonyesho ya bidhaa za viwanda vya ndani yanayoendelea katika viwanja vya Sabasaba, jijini Dar es Salaam.

"Kuendelea kununua bidhaa kutoka nje ambazo zina viwango vya chini kuliko zile zinazozalishwa nchini ni kuhujumu juhudi za serikali za kuvutia uwekezaji katika viwanda nchini," alisema.

Alisema EPZA, kwa niaba ya serikali imekuwa mstari wa mbele kuweka mazingira wezeshi ili kuvutia uwekezaji zaidi nchini.

Katika kusimamia uzalishaji, alisema viwanda vilivyoanzishwa chini ya EPZA vinazalisha bidhaa zinazokidhi viwango na ushindani wa kimataifa.

Maziku alisema, kwa kupitia uwekezaji katika maeneo maalum kwa ajili ya mauzo nje ya nchi yaani EPZ, asilimia 80 ya bidhaa zinauzwa nje ya nchi na 20 zinauzwa ndani ya nchi.

Alisema zinazouzwa katika soko la ndani zina ubora sawasawa na zinazouzwa nje ya nchi.

Maziku alisema kwa wananchi kuendelea kununua bidhaa kutoka nje ya nchi ambazo ubora wake ni mdogo kuliko zile zinazozalishwa nchini ni kutoitendea haki nchi na kuikosesha mapato.

Pia, alisema viwanda ambavyo vipo chini ya EPZA ambavyo huzalisha bidhaa za kilimo kwa ajili ya kuuza nje ya nchi, vinachangia kwa kiasi kikubwa kuongeza pato katika sekta ya kilimo.

Alisema fursa hiyo imewafanya wakulima kujihakikishia soko la uhakika la mazao yao na kuongeza kipato na kuchangia uchumi wa nchi.

Meneja Uhamasishaji Uwekezaji wa EPZA, Grace Lemunge, alisema mamlaka hiyo imetumia fursa ya maonyesho ya bidhaa za viwanda vya ndani kuhamasisha Watanzania kununua bidhaa za kitanzania ili kuviendeleza zaidi viwanda vya ndani.

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

ISO 9001: 2015 IMETHIBITISHWA

# TAARIFA KWA UMMA
# MABORESHO YA MIFUMO YA UKUSANYAJI KODI

**Dar es Salaam, Desemba 7, 2020**

Itakumbukwa kwamba Mamlaka ya Mapato Tanzania ("TRA" au "Mamlaka") imeendelea kuboresha mifumo yake ya ukusanyaji kodi kila inapobidi. Lengo ni kurahisisha na kukuza ulipaji kodi wa hiari kwa wafanyabiashara na kuongeza ufanisi. Kama sehemu ya maboresho hayo, kwa sasa TRA imeboresha mfumo wake wa uwasilishaji ritani za kodi (**e-Filling**) ikiwemo ritani ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT). Aidha, maboresho haya yameenda sambamba na uboreshaji wa mfumo wa EFDMS kwa kuweka programu mpya ijulikanayo kama **Protocol 2.1**.

Kufuatia maboresho yaliyofanyika kwenye ritani ya VAT, inayowasilishwa kwa njia ya kielektroniki kupitia mfumo wa **e-Filling**, imebainika kuwa kuna baadhi ya mashine za EFD, ambazo hazina uwezo wa kutoa risiti ambazo zitaweza kufanyiwa uhakiki na mfumo moja kwa moja (**automatically**). Mabadiliko haya ni ya msingi na ni jambo la lazima, ambapo kila mfanyabiashara anapaswa kuwa na mashine ya EFD inayoendana na mahitaji ya mfumo huu ulioboreshwa ambao unalenga ukusanyaji wa mapato ya Serikali wenye tija.

Kwa msingi huo hapo juu, Mamlaka inapenda kuwajulisha wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla kuwa katika **kipindi kisichozidi siku thelathini (30)** tangu **tarehe ya tangazo hili**, kila mfanyabiashara ambaye kwa sasa anatumia mashine inayotoa risiti ambazo haziwezi kuhakikiwa na mfumo ulioboreshwa anapaswa kununua na kutumia mashine mpya (zenye **Protocol 2.1**) zinazosambazwa na Wakala wa EFD aliyethibitishwa na TRA. Aidha, mashine za zamani ziwasilishwe katika Ofisi za TRA zilizopo karibu nawe kwa hatua zaidi.

Sambamba na mabadiliko hayo, tunapenda kuwajulisha kuwa, katika mfumo wa sasa ulioboreshwa, wafanyabiashara wanaweza kutumia kompyuta, **Point of Sale (POS)**, na mashine nyingine zenye uwezo wa kuunganishwa na mfumo wa EFDMS. Katika mazingira haya, mfanyabiashara hahitajiki kununua mashine ya EFD na badala yake atatumia mashine tajwa kuunganishwa kwenye mfumo ulioboreshwa. Kwa hiyo, wale watakaochagua utaratibu huu watahitajika kuwasiliana na Ofisi za Mamlaka zilizopo karibu nao ili waweze kuelimishwa zaidi juu ya namna mashine zao zitavyounganishwa na mfumo wa sasa ili waweze kuwasilisha taarifa zote zinazohitajika kwa ajili ya kulipa kodi stahiki. Vile vile, tunachukua fursa hii kuwakumbusha walipakodi wetu kuwa fedha za kununua mashine za EFD zitagharamiwa na Serikali kwa kuruhusiwa kudai kwenye ritani za VAT ambazo huwasilishwa kila mwezi kwa mujibu wa **Jedwali la Saba (7) la Kanuni za Sheria ya Usimamizi wa Kodi za Mwaka 2016**. Kwa wale ambao hawajasajiliwa na VAT gharama za kununua mashine zitarejeshwa kwa kupunguzwa kwenye mapato yao kwa kuzingatia matakwa ya **Kifungu cha 11(2) cha Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332**.

Mwisho, tungependa kuweka bayana kuwa, baada ya muda wa **siku thelathini (30)** uliobainishwa kwenye tangazo hili kumalizika, wafanyabiashara ambao watakuwa hawajatekekeleza maelekezo haya watachukuliwa kuwa ama, hawana mashine za EFD au hawatumii mashine za EFD, ambapo ni kinyume cha sheria, hali ambayo itailazimu TRA kuchukua hatua stahiki za kisheria ikiwemo kuwapa hati za makosa na kutozwa adhabu na faini. Ni matumaini yetu kuwa kila mmoja wetu atazingatia maelekezo haya muhimu na kuyatekeleza ipasavyo ndani ya muda uliowekwa ili kuepuka adhabu na usumbufu usio wa lazima.

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

**Imetolewa na**

**MKURUGENZI WA ELIMU NA HUDUMA KWA MLIPAKODI**

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# SUK ianze utatuzi masuala yanayowasibu wananchi

**RAIS** wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, amemteua Mwenyekiti wa ACT -Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK), visiwani humo.

Rais Mwinyi anaelekea kukamilisha nia yake, maana tangu mwanzo alitangaza azma yake ya kuunda serikali ya ushirika inayohusisha wapinzani, hongera kwa kufikia azma hiyo.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa ni muhimu na ndiyo njia pekee ya kuwashirikisha wanasiasa wengine kwenye uongozi bila kujali kuwa walikuwamo kwenye mchakato wa uchaguzi mkuu, lakini hawakuchaguliwa.

Hongera serikali, ACT-Wazalendo na Wazanzibari kwa kushirikiana na kuchukua hatua hiyo, inayoonekana na kukubaliwa na wengi kuwa inafaaa kupunguza mkwamo wa kisiasa miongoni mwa wananchi.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa kama ilivyoelezwa na viongozi wakuu wa serikali inalenga kuleta amani, maelewano, upendo na kuongeza ushirikiano miongoni mwa Wazanzibari.

Inafahamika kuwa SUK inaundwa kwa mujibu wa katiba ya Zanzibar inayotaka kuwapo na serikali ya umoja huo inayokuwa na wapinzani pamoja na chama tawala. Lakini utashi wa kisiasa nao muhimu kufikia azma hiyo.

Tunaomba serikali hiyo ianze sasa kuwasaidia na kuwatatulia wananchi changamoto zao.

Mathalani, ihakikishe kunakuwa na usafiri wa uhakika na wa kisasa baina ya Unguja na Pemba pamoja na Dar es Salaam.

Iwe ni wa ndege, meli au boti ziendazo kasi tukiamini kuwa hatua hiyo ni ya muhimu katika utekelezaji wa maazimio na yale yaliyomo kwenye mikakati ya kuwasaidia wananchi hasa kuondokana na changamoto sugu ya usafiri.

Wanaounda serikali ya umoja wa kitaifa wanapaswa kuanzia sasa kuwa na mtizamo mpya wa kujenga na kuendeleza amani, mshikamano, kuponya majeraha na kudumisha umoja wa kitaifa.

Halikadhalika, kuenzi na kuendeleza upendo badala ya utengano na hisia za kujiona kuwa sisi Wapemba au Wazanzibari au Waunguja. Ni muda wa kuponya majeraha na kuachana na fikra kuwa wapo wanyonge na wengine wenye nguvu.

Tunaishauri serikali ya umoja kuwa na sera ya kitaifa ya kuendelea kuwalinda wananchi, kuwainua kiuchumi, kisiasa na kuwakumbuka majeruhi hasa wale walioumizwa na harakati za kisiasa kwenye uchaguzi mkuu, kabla ya kufikia maamuzi hayo ya kuungana na kuwa na serikali ya pamoja.

Tunaona kuwa huu ndiyo wakati wa kujenga taifa kwa kuwa na mikakati ya kunyanyua kilimo, kuboresha viwanda, utalii, biashara, bandari na sekta ya uvuvi.

Tunaishauri SUK kuwa na mkakati kabambe wa kuanzisha viwanda vidogo, vya kati na vikubwa na kuwa na mipango endelevu inayoisimamia uchumi na maendeleo.

Viongozi wa SUK wana wajibu wa kuona na kuhakikisha kuwa vijana wanainuliwa. Wanakuwa na hali bora zaidi na wananchi wananufaika na kuwa na maisha bora.

Tunaamini kuwa serikali hiyo ya ushirikiano inapoongoza wananchi itakuwa kama chombo kinachoumizwa na masuala mbalimbali yanayowagusa wananchi.

Mambo hayo ni kuanzia umaskini, maisha duni, lakini pia vita na chuki za muda mrefu zinazohusu upande mtu anapotoka iwe Unguja au Pemba.

Tunawaombea amani, mshikamano na mafanikio katika kuwatumikia wananchi ambao daima wana kiu ya maendeleo na si harakati za kisiasa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Christina Mwakangale

# Ubakaji watoto watuhumiwa hamkuvaa viatu vya 'uzazi'?

**WAHENGA** husema uchungu wa mwana aujuaye mzazi. Lakini pamoja na hayo ukweli ni kwamba kila mmoja akumbuke kuwa alikuwa mtoto na sasa ni mtu mzima, hivyo anapaswa kumsaidia mtoto ili akue na kufikia hatua za kujitegemea na kumudu maisha yake.

Hivyo ndivyo naweza kusema kufuatia wiki moja ya matukio mfululizo ya watuhumiwa wa ubakaji wanafunzi na watoto kujaza vichwa vya habari.

Ikumbukwe elimu kwa mtoto ndiyo msingi wa maisha, ukiwa ni msuli anaojifunga kukabiliana na kupambanua changamoto na matatizo kuanzia uchumi, afya na mikiki ndani ya jamii.

Kilichotokea karibuni ni pamoja na mwalimu wa sekondari Vwawa wilayani Mbozi, mkoani Songwe kushikiliwa kwa tuhuma za kunaswa na mwanafunzi nyumbani kwake katika mazingira yanayohusishwa na ubakaji.

Aidha, Mwenyekiti wa Kijiji cha Ijinga huko Magu, mkoani Mwanza, kutuhumiwa kumpa ujauzito mwanafunzi wa darasa la sita wa shule ya Ijinga, anayedaiwa kuwa na miaka 15.

Tukio jingine ni mtoto wa miaka sita huko Arusha, kubakwa hadi kufa wakati mwingine wa miaka 12 kutoka wilayani Serengeti naye alibakwa na kujeruhiwa vibaya.

Hiyo ni orodha iliyotolewa na Chama cha Wanahabari Wanawake (TAMWA) kuhusu mwenendo wa ubakaji katika mikoa mbalimbali.

Ni taarifa zinazotolewa kuelekea kilele cha maadhimisho ya kupinga ukatili wa kijinsia duniani kinachofikiwa kesho Jumatano Desemba 10 na mwaka huu kauli mbiu ni 'mabadiliko yanaanza na mimi'.

Ni vyema kauli hiyo ikagusa jamii na kubadilika ili kuachana na vitendo hivyo.

Takwimu za hivi karibuni za Umoja wa Mataifa (UN), zinaonyesha kuwa wasichana na wanawake milioni 243 duniani, walitendewa ukatili na ndugu, marafiki au majirani wanaowazunguka.

Kwa hiyo ni wakati wa kuwalinda wanawake, watoto na wahitaji ambao wapo kwenye hatari ya kubakwa au kunyanyaswa kutokana na udhaifu au hali ya maumbile yao.

Lakini si hivyo tu, vikwazo wanavyokumbana navyo wasichana ambao bado wapo shuleni, vinatakiwa kuondolewa ili kufikia malengo yao.

Baadhi ya vikwazo ni kama kukosa msaada na fedha kutoka kwa wazazi na walezi ili kununua mahitaji ya muhimu na kujikimu wakiwa shuleni. Wasichana wengi hulazimika kuingia kwenye ngono ututoni kupata fedha za kununulia mafuta, sabuni, daftari, chakula na taulo za kike kwa sababu hawana wala wa kuwasaidia.

Wengine wanalazimika kuwa na uhusiano na walimu, madereva wa pikipiki, wafanyabiashara na hata jamaa zao wa karibu ili kuwasaidia fedha za kujikimu.

Tukirejea kwenye suala la ubakaji na uharibifu wa watoto tunajiuliza hivi wahusika hao hawana uchungu na watoto wawe wa kuwazaa au wa ndugu zao?

Kwa sababu ukiangalia takwimu za wanaotuhumiwa kufanya vitendo hivyo na ambao hata wamekwishapewa hukumu baada ya kuthibitika na kutiwa hatiani mahakamani, wana umri wa utu uzima kuanzia miaka 25 na kuendelea wengine wakiwa ni wazee.

Matukio hayo yanaonyesha namna gani jamii bado inahitaji elimu, kutambua mtoto awe wa kike au wa kiume ana haki ya kusoma na kukamilisha malengo kama ilivyo kwa mtoto wa kiume.

Pia watenda makosa au watuhumiwa wajaribu kuvaa viatu vya mzazi, je, ingekuwa ni mwanawe anabakwa pengine hata kufa angejisikiaje?

Mtoto wa mwenzio ni wako, waacheni watoto wa kike wakue, msiwajeruhi, kuwaathiri kisaikolojia na kuwaangamiza. Walindeni wadogo hawa wasome, wakue na watimize ndoto zao.

## HABARI KITAIFA

# Takwimu za kilimo zatajwa katika kupunguza umaskini

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

OFISI ya Taifa ya Takwimu (NBS) imesema kama sekta ya kilimo itaendelea kutoa mchango kwa maendeleo ya jamii na kiuchumi hasa kwenye kuongeza kipato, kuondoa umaskini.

Pia hatua hiyo itasaidia kuimarisha upatikanaji na usalama wa chakula kwa nchi nyingi za bara la Afrika na takwimu katika eneo hilo zinatakiwa kuendelea kufanyika.

Kauli hiyo ilitolewa na Meneja wa Takwimu za Kilimo wa NBS, Titus Mwisomba, wakati akizungumza na wadau wa kilimo wakati wa kikao cha Mpango Mkakati wa Kuboresha na kuendeleza Takwimu awamu ya pili (ASSP ll) Manispaa ya Morogoro.

Katika kilichoandaliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali ya Marekani, Benki ya Dunia, Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) na Umoja wa Ulaya(EU) na kushirikisha wadau wa kilimo.

Mwisomba alisema lengo la kukutana na wadau wa kilimo ni kupitia mpango wa kwanza wa ASSP l ambao ulikuwa wa miaka mitano uliomalizika, na kwamba kikao kizi hicho kinatarajiwa kutoa mawazo kutoka kwa wadau wa taasisi binafsi, ili yale yatakayofikiwa kupelekwa kwa watoa maamuzi. Hata hivyo, alisema mpango umefanikisha kupatikana kwa takwimu za kilimo na kutokana na washiriki kushirikishwa kwa dhati katika kuandaa mnyororo huo wa kuboresha na kuimarisha, takwimu za kilimo, mvuvi na mifugo.

"Zipo baadhi ya changamoto zilizojitokeza katika mpango wa awamu ya kwanza kama upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa programu mbalimbali kwa wakati na ushiriki wa wadau wachache, umetusaidia kujenga ule mpango wa pili," alisema Mwisomba.

Alisema kutokana na mafanikio ya mpango wa kwanza, kwa sasa wanawategemea wadau hao kutoa maoni yao yatakayosaidia kuboresha upatikanaji wa takwimu sahihi na zitazoenda na wakati hasa wa sekta binafsi za kilimo na mifugo.

Mchambuzi wa masuala ya Chakula na Lishe kutoka FAO, Fadhili Mtengela, alisema mpango mkakati huo umesaidia kufanyika kwa utafiti wa kilimo, mifugo na uvuvi kwa mwaka 2014 hadi 2017, Sensa ya mwaka 2019/2020, utafiti wa makadirio ya uzalishaji wa chakula na uimarishaji wa takwimu za kiutawala (ARDS).

Alisema takwimu zilizopatikana kutokana na utafiti huo zinaweza kutumika na serikali pamoja na wadau katika utungaji sera, kupanga mipango, kupima na kusimamia miradi ya maendeleo ya sekta ya kilimo nchini.



Mkuu wa Idara ya Wateja Binafsi na wa Kati wa Benki ya NCBA, Julius Konyani (katikati), akipeana mikono na Ofisa Masoko wa GSM, Fatma Farah, baada ya uzinduzi wa promosheni ya "Nenda shopping na punguzo kutoka NCBA", wateja wa benki hiyo wataweza kupata punguzo la asilimia 10% watakapofanya manunuzi kupitia maduka ya GSM kote nchini kwa kipindi hiki cha msimu wa sikukuu. Kulia ni Mkuu wa Masoko, Mawasiliano na Utaifa wa Benki, Caroline Mbaga, hafla hiyo ilifanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# VETA yamkabidhi mhitimu cherehani

**Na Beatrice Moses**

MHITIMU mwenye uhitaji maalum, Neema Chole, katika Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), amezawadiwa cherehani baada ya kufaulu masomo ya ushonaji vizuri.

Mkuu wa Chuo hicho, Joseph Mwanda, akizungumza mwishoni mwa wiki kwenye mahafali ya kumaliza mafunzo ya ufundi stadi na huduma daraja la pili na tatu, iliyofanyika jijini Dar es Salaam, alisema Neema amefulu kupata alama B, na VETA imeamua kumzawadia cherehani ambayo anaweza kuitumia vizuri licha ya kuwa ana ulemavu wa miguu.

"Tunamzawadia cherehani maalum kutokana na juhudi zake kata kujifunza, amefanya vizuri imekuwa ni kama taarifa kwa wazazi wanaoficha watoto wenye ulemavu kwa kuamini kuwa hawawezi kushiriki kwenye maendeleo, wanatakiwa kuwaendeleza kielimu ili wapate ujuzi kama huo utakaowasaidia kujipatika kipato," alisema Mwanda.

Aisema chuo hicho kinaendelea kuboresha mazingira ya kupokea wanafunzi wa aina mbalimbali wakiwamo wenye uhitaji maluum na kwa sasa wapo 21 wakiwamo wenye ulemavu wa viungo na akili, waweze kupata nafasi nzuri ya kujifunza fani wanazopenda au wanazomudu kulingana na aina ya ulemavu walionao.

Naibu Mkurugenzi wa Temeke, Deogratus Lukomanya, alimkabidhi Neema zawadi hiyo na meza maalum iliyotengenezwa na wanafunzi wenye uhitaji wenye ulemavu wa akili.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa zawadi hiyo, Neema ambaye alijiunga na mafunzo hayo baada ya kuhtimu kidato cha nne katika Sekondari ya Jangwani, jijini Dar es Salaam, aliushukuru uongozi wa chuo hicho na kueleza furaha yake ya kuwa miongoni mwa wanafamilia wa VETA.

Kaka Mkuu wa wanafunzi wenye ulemavu, Paulo John, akizungumza na gazeti hili, alisema wanafurahi kupata mafunzo ya ufundi mbalimbali na kuwashauri wazazi wenye vijana wenye ulemavu kuwasiliana na VETA ili wawapeleke kupata mafunzo hayo.

"Umeona Neema amehitimu nasi tumefurahishwa na juhudi zake ndipo tukaamua kumtengenezea meza maalum ya kuwekea cherehani yake, ili aweze kushona nguo za wateja wake vizuri, tumefurahi," alisema.

Wahitimu katika mahafali hayo ni 616, miongoni mwao wanawake ni 153.




# Bima kwa wateja CRDB yamkuna Kamishna TIRA

**Na Mwandishi Wetu**

KAMISHNA wa Mamlaka ya Bima (TIRA), Dk. Mussa Juma, ameipongeza Benki ya CRDB kwa kuanzisha huduma ya bima ambatanishi ya maisha ijulikanayo "KAVA Assurance" kwa wateja wenye akaunti katika benki hiyo, kwa kushirikiana na kampuni ya bima ya Sanlam Tanzania.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi huo, Dk. Mussa alisema kuanzishwa kwa huduma hiyo ya bima kwa akaunti za wateja kutaongeza chachu ya matumizi ya huduma za kifedha pamoja na kuongeza uelewa wa huduma za bima kwa Watanzania.

"Huduma hii ya Bima Ambatanishi katika akaunti za wateja imekuja wakati mwafaka, ambapo Mamlaka ya Bima imejikita katika kuhakikisha Watanzania wote wanafikiwa na huduma za kifedha ikiwamo huduma za bima," alisema Dk. Mussa, huku akiitaka Benki ya CRDB na Sanlam kujikita katika kutoa elimu kwa wateja ili kuongeza uelewa zaidi.

Akielezea kuhusiana na huduma hiyo KAVA Assurance, Mkurugenzi wa Wateja Wadogo na Wakati wa Benki ya CRDB, Boma Raballa, alisema kupitia huduma hiyo wateja zaidi ya milioni 3 wenye akaunti Benki ya CRDB watakuwa wakipata malipo ya gharama za mazishi mteja anapofariki, gharama za usafirishaji mwili mteja anapofariki nje ya nchi na mkono wa pole pale mteja anapopata ajali inayopelekea ulemavu wa maisha.

"Endapo mteja atapata changamoto hizi basi benki itatoa mkono wa pole kwa ndugu ambapo kwa wateja wa kawaida mteja atapewa kiasi cha shilingi milioni 2, wateja maalum wao ni shilingi milioni 5 na shilingi milioni 15 kwa wanaoishi nje ya nchi," alisema Raballa, huku akibainisha kuwa huduma hiyo ni ya kumwongezea mteja thamani na hakutakuwa na gharama za aina yoyote kwa wateja.




Kamishna wa Mamlaka ya Bima (TIRA), Dk. Mussa Juma (kushoto) na Ofisa Biashara Mkuu wa Benki ya CRDB, Dk. Joseph Witts, wakizindua rasmi huduma ya bima ambatanishi ya Benki ya CRDB "KAVA Assurance", ambayo inawawezesha wateja wa ndani na nje ya nchi (diaspora) kupata mkono wa pole wa Sh. milioni 2 hadi Sh. milioni 15 kwa matatizo ya msiba au ajali. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wajasiriamali washauriwa kutumia Posta kuuza bidhaa

**Na Mwandishi Wetu**

WAJASIRIAMALI nchini wameshauriwa kutumia Shirika la Posta kutangaza na kuuza bidhaa zao ndani na nje ya nchi.

Shirika hilo linafanya huduma hizo kwa kujisajili bure kwenye duka lao la mtandao na kuwarahisishia kuuza bidhaa zao kirahisi, huku wateja wakifikishiwa mzigo waliounununua popote walipo.

Meneja biashara za mtandao wa shirika hilo, Amina Salum, alisema hayo alipokuwa akizungumza na gazeti hili katika maonyesho ya viwanda yanayoendelea jijini Dar es Salaam.

"Duka la mtandaoni la shirika linaitwa Posta Shop Tanzania, lipo kwa ajili ya kusajili wajasiriamali na wafanyabiashara mbalimbali wenye bidhaa zao wakiwamo Watanzania na wa nje ya nchi."

Alisema mpaka sasa shirika limesajii wateja 90 ambao wapo katika mtandao.

Amina alisema, hivi karibuni duka hilo litazinduliwa rasmi kwa kuwa shirika linataka kushirikiana na Tantrade kwa ajili ya kupata wauzaji nje ya nchi.

Alisema wafanyabiashara wengi hawana pa kuuzia bidhaa zao na duka hilo litawarahisishia wateja kwa kuwa wanaweza kununua bidhaa wakiwa nyumbani mwao.

"Posta inauza na kumpelekea mfanyabiashara pesa zake kisha kuwapelekea wateja majumbani mwao mara wanunuapo bidhaa hizo," alisema.

Alisema faida ya duka hilo linaondoa usumbufu kwa wananchi kwa kutumia muda mchache kwa kupitia duka hilo.

"Kupitia duka hilo wananchi watanunua bidhaa tofauti kwa wakati mmoja na kulipia hapo hapo walipo na Posta itakuletea popote," alisema.

Aliwataka wafanyabiashara wanaotaka kujisajili kuingiza bidhaa hizo ikiwamo bei, uzito na aina tofauti ili kuwezesha wateja kujua wanataka nini na bei.

Pia, wateja na wafanyabiashara kutumia duka hilo kwa kuwa ni la uhakika tofauti na biashara nyingine za mitandaoni ambazo zimekuwa zikiwaliza wengi kwa kufanya udanganyifu.

# TARURA yatumia bil. 74/- barabara za lami Mpanda

**Na Thobias Mwanakatwe**

WAKALA wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), kupitia mradi wake wa Uimarishaji wa Halmashauri za Miji (ULGSP), umetumia shilingi billioni 7.4 kutekeleza mradi wa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami katika Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda mkoani Katavi.

Barabara hizo zenye urefu wa kilometa 7.7 zimesaidia kurahisisha usafiri kwa urahisi kwa wananchi wa mji wa Mpanda.

Kaimu Mratibu wa TARURA Mkoa wa Katavi, Mhandisi Henry Mtawa, alisema hayo jana wakati wa ukaguzi wa miradi mbalimbali iliyotekelezwa katika mkoa huo tangu kuanzishwa kwa TARURA.

Mtawa alisema ujenzi wa barabara hizo ulianza mwaka 2017 na kukamilika mwaka 2019, na kwamba umesaidia kuboresha mandhari ya mji huo, ambapo kipindi cha usiku wananchi wanaendelea na kazi zao kutokana na taa zilizowekwa barabarani.

Alisema kutokana na mradi huo, wakazi wa Halamashauri ya Manispaa ya Mpanda wameondolewa kero ya muda mrefu ya mafuriko katikati ya mji hasa kipindi cha masika, na kupitia mradi huu maji yameweza kutengenezewa njia na sasa hakuna tena mafuriko kwa wananchi.

Juma Phinias, mkazi wa Mtaa wa Nsemulwa, alieleza kuwa kipindi cha nyuma kabla ya barabara hizo za lami, kulikuwa na vumbi kali kipindi cha kiangazi huku kukiwa na matope kipindi cha masika, lakini kwa sasa wananchi wananufaika na mradi huo.

"Tunaishukuru sana serikali kwa ujenzi wa barabara hii, kwa sasa tunafanya shughuli zetu katika kipindi chote cha mwaka pamoja na biashara ndogo ndogo zinaendelea kufanyika ata usiku," alisema Juma.

Aidha, licha ya ujenzi wa barabara hizo, TARURA katika Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda imefanikisha ujenzi wa daraja katika barabara ya Mkumbo inayounganisha kata ya Nsemula pamoja na Kashaulili lililogharimu shilingi milioni 163 na kutatua kero za kudumu kwa wakazi wa kata hizo mbili hususani kwa kipindi cha masika.

Akizungumzia uwapo wa daraja hilo mkazi wa eneo la Mtaa wa Mnazi Mmoja, Kata ya Uwanja wa Ndege katika Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda, Nasir Mikidadi, alisema awali kulikuwa na daraja dogo ambalo lilikuwa kero kwa wakazi wa mitaa hiyo katika kipindi cha mvua kwani maji yalikuwa yanapita juu ya daraja na kusababisha kukwama kwa shughuli zao pamoja na watoto kushindwa kufika shuleni, ameongeza kuwa uwepo wa daraja hilo la kudumu ni utatuzi tosha wa kero ya muda mrefu.

# Wauguzi wadaiwa kupotosha

**Na Mwandishi Wetu**

WAUGUZI wasio na uelewa wa kutosha kuhusu ugonjwa wa kisukari wamedaiwa kuwa chanzo cha kuwavuruga wazazi na walezi wa watoto wanaoishi na tatizo hilo.

Hayo yamebainika wakati timu ya wataalamu wa magonjwa yasiyo ya kuambukiza kutoka Chama cha Ugonjwa wa Kisukari Tanzania (TDA), walipokutana na baadhi ya wagonjwa kutoka mikoa ya Dar es Salaam na Pwani, katika kituo cha tiba cha kliniki ya kisukari Hospitali ya Temeke, mwishoni mwa wiki.

"Mmekuwa mkituchanganya kwa sababu mnachotufundisha hapa tukienda kwenye vituo vyetu, wauguzi wamekuwa wakitupinga na kutaka tuwasikilize wao," alisema Bakari Hamad kutoka mkoa wa Pwani alipokuwa akielezea changamoto wanazozipata.

Alitoa mfano kwenye maelezo ya wataalamu hao waliambiwa ni lazima kila siku kuwachoma sindano za 'insulini' watoto wao wanaougua kisukari, lakini kwenye vituo vyao wauguzi wanawaambia iwapo watapunguza kiwango cha vyakula vya wanga na sukari wanaweza kuacha kuwachoma kichocheo hicho.

Mtaalamu wa Magonjwa ya Kisukari kwa Watoto wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Dk. Honesta Kipasika, alionya akisema watoto waliozaliwa na ugonjwa wa kisukari wanapaswa kuchoma insulin maisha yao yote kulingana na maelekezo ya daktari na siyo suala la kula vyakula.

"Watoto hawa wanaugua kisukari cha aina ya kwanza ambacho kinatokana na kongosho kutokuwa na uwezo wa kuzalisha insulini ili miili yao itumie sukari pamoja na vyakula vya wanga," alisema.

Dk. Kipasika alisema wanaougua kisukari cha aina hiyo ni lazima kuongezewa insulin muda wote kwa kuchomwa sindano, tofauti na wanaugua kisukari cha aina ya pili, hao huweza kupunguza tatizo kwa matumizi makubwa ya vyakula vya wanga pale uchunguzi wa kitabibu unapothibitisha uwezekano huo kulingana na uwezo wa kongosho.

Utata huo umekuja katika maadhimisho ya mwaka huu ya ugonjwa wa kisukari yalibeba kaulimbiu: 'Wauguzi na ugonjwa wa kisukari' wakiwahimiza kuwa na uelewa wa kutosha kuhusiana na maradhi hayo kwa kuwa ndiyo waliokaribu zaidi na wagonjwa.

Mratibu wa Miradi wa Shirikisho la Vyama vya Magonjwa Yasioambukiza Tanzania (TANCDA), Happy Nchimbi, alisema utafiti wao unaonyesha kuwa bado baadhi ya wauguzi wanahitaji kujengewa uwezo wa elimu ya magonjwa hayo ili watekeleze kazi zao kikamilifu.

Alisema TANCDA kwa kushirikiana na TDA wanaendesha mafunzo na hata kuwatembelea wauguzi kwenye vituo vyao ili kuwaongezea ufahamu wa magonjwa hayo.

Mwelimishaji wa TDA, Elizabeth Likoko, alifafanua kuwa insulini wanayochomwa watoto wanaougua kisukari inakuwa ni "ufungua unaoruhusu glukosi au sukari kuingia kwenye seli zote ili itumike kama nishati ya kuupatia mwili nguvu."

Aliongeza kuwa kila mtu mwenye kisukari cha aina ya kwanza anahitaji kutumia insulini ili imsaidie kudhibiti viwango vya sukari kwenye damu kwa sababu mwili wake hauwezi kuizalisha.

# Wazazi waonywa kitupiana watoto

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WAZAZI wametakiwa kuacha tabia ya kutupiana watoto kwani ni njia mojawapo inayosababisha watoto hao kukosa haki zao za msingi na hatimaye kudhalilishwa.

Akizungumza katika maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Udhalilishali, yaliyofanyika katika Uwanja wa Gombani Chakechake Mkuu wa Wilaya hiyo, Rashid Hadid Rashid, alisema kuwa, ipo haja ya kuwatunza watoto ili kupata taifa bora la baadaye.

Alisema tabia ya kutupiana watoto kwa baadhi ya wazazi, sio jambo jema na linakera sana kwa sababu ndio chanzo kikubwa cha watoto hao kufanyiwa udhalilishaji kutokana na kuwa wanakosa haki zao za msingi.

"Vijana wa siku hizi kazi yao ni kuoa na kuacha, kitanda kimoja anaweza kuolea wake saba… hii inasikitisha sana kwa sababu wanawaacha watoto wanasambaratika, kwani wengi wao wanakosa huduma stahiki," alisema.

Alieleza kuwa suala la udhalilishaji ni kubwa na linaendelea kufanyika katika jamii, hivyo ni vyema wakashirikiana pamoja katika kuhakikisha wanaondosha kadhia hiyo na watoto wanabaki salama.

Alisema siku 16 za kupinga udhalilishaji ni muhimu sana kwao, kwani kilikuwa ni kipindi maalumu cha kutafakari na kufanya kampeni za makusudi juu ya kupinga ukatili na udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto.

"Lengo la kuwapo siku hii ni kuongeza ushawishi, kubadilishana taarifa za uzoefu, kujenga uwezo wa pamoja, matumizi ya rasilimali zilizopatikana na kuunganisha nguvu kati ya serikali na asasi za kijamii katika kuhamasisha, kuelimisha, kukemea na kuchukua hatua za kisheria," alieleza.

Alisema Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), ni wadau wakubwa wa kupambana na udhalilishaji, ambao wameamua kuadhimisha siku hii na kupaza sauti zao kwa wanyonge , jambo ambalo litasaidia kwa kiasi kikubwa kuliondosha janga hilo.

Mratibu wa TAMWA Pemba Fat-hiya Mussa Said, alisema wanaadhimisha siku hiyo, ili jamii ibadili tabia na iachane na udhalilishaji ambao umekuwa ni janga zito linalowakabili wanawake na watoto.

Aliiomba jamii isiwafiche watuhumiwa, badala yake wawafikishe katika vyombo vya sheria ili watiwe hatiani.

# PM aagiza hospitali itoe huduma Des. 20

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kushoto), akimsikiliza Mkurugenzi wa Masoko wa kiwanda cha sukari cha Kilombero, Fimbo Butala, akizungumza kuhusu sukari inayozalishwa na kiwanda hicho, wakati alipotembelea banda lao katika maonyesho ya 5 ya bidhaa za viwandani zinazozalishwa nchini, yaliyofanyika viwanja vya Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa ya Mwalimu Nyerere, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amekagua umaliziaji ujenzi wa Hospitali ya Uhuru unaoendelea wilayani Chamwino, jijini Dodoma na kuagiza huduma zianze kutolewa ifikapo Desemba 20, mwaka huu.

Pia, alikagua hospitali hiyo jana na kusema vifaa vyote zikiwamo samani na vifaa tiba vinavyohitajika kuwapo vipelekwe na vifungwe ili huduma zianze mara moja.

"Tunakusudia kumwomba mheshimiwa Rais John Magufuli, aje kuzindua hospitali hii kabla ya Desemba 30, mwaka huu, hakikisheni vifaa vyote vinaletwa na kufungwa, huduma zianze kutolewa," ilisema taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Iliongeza kuwa wiki iliyopita Rais Magufuli aliahirisha maadhimisho ya sherehe za miaka 59 ya Uhuru zilizotarajiwa kufanyika Desemba 9, 2020 na kuelekeza zaidi ya Sh. milioni 835.5 zilizotengwa kwa ajili ya sherehe za hizo zitumike kununulia vifaa mbalimbali kwa ajili ya Hospitali ya Uhuru.

Pia, Rais aliagiza fedha hizo zitumiwe kwa ajili ya ujenzi wa uzio wa kuzunguka hospitali hiyo, pamoja na ujenzi wa barabara ya kuingilia hospitalini hapo.

Hadi kufikia sasa ujenzi wa hospitali hiyo umegharimu Sh. bilioni 4.2.

Januari 2019, wakati akipokea gawio la hisa za kampuni ya simu ya Airtel, Rais Magufuli aliagiza kiasi Sh. bilioni 2.41 zilizotolewa na kampuni hiyo zitumike katika ujenzi wa hospitali hiyo.

Novemba 20, 2018, aliagiza Sh. milioni 995.18 zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya maadhimisho ya miaka 57 ya Uhuru, zitumike kujenga hospitali hiyo ambayo kwa sasa ujenzi umefikia hatua za umaliziaji.

Kaulimbiu ya maadhimisho ya miaka 59 ya Uhuru kwa mwaka huu ni: 'Miaka 59 ya Uhuru na Miaka 58 ya Jamhuri: Tanzania yenye Uchumi Imara Itajengwa na Watanzania Wenyewe, Tufanye Kazi kwa Bidii, Uwajibikaji na Uadilifu.'

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, aliishukuru serikali kwa kuboresha huduma za afya mkoani Dodoma ikiwamo ujenzi wa hospitali hiyo.

Alisema mahitaji ya wataalamu wa afya wakiwamo madaktari katika mkoa ni 2,505 huku waliopo ni 1,767, na kuiomba serikali iwasaidie kutatua changamoto hiyo kwa kuajiri wataalamu wa kutosha.

Alisema Hospitali ya Benjamin Mkapa inakabiliwa na tatizo la ukosefu wa nyumba za wataalamu, aliomba msaada wa ujenzi wa nyumba hizo ili kuwawezesha watoa huduma hao kuwa na makazi karibu na hospitali.

# Bil. 1.6/- kutatua kero ya maji Chalinze

Na Thobias Mwanakatwe

SERIKALI imetoa Sh. bilioni 1.6 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Kata ya Kibindu Wilaya ya Bagamoyo mkoani Pwani.

Hayo yalielezwa jana na Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Zainab Kawawa, wakati wa ziara ya Mbunge wa Chalinze, Ridhiwan Kikwete, alipokwenda kuzungumza na wananchi wa kata hiyo kuhusu kero mbalimali zinazowakabili.

Kawawa akizungumza mbele ya wananchi wa kijiji cha Kwamduma alieleza kuwa, serikali imejizatiti kutoa kiasi hicho cha fedha ili kuhakikisha maji yanawafikia wananchi wa Kibindu, hivyo alimhakikishia Ridhiwan na wananchi kuwa mradi utakamilika mapema ili wananchi wapate majisafi na salama.

Alisema miradi hiyo inatarajiwa kwa pamoja kutoa lita zisizopungua milioni 3.5, hivyo kutatua kero ya maji katika Kata ya Kibindu.

Miradi hiyo itakapokamilika, inatarajia kuhudumia watu wanaoishi katika eneo la Kibindu na vitongoji vya kata hiyo na za jirani.

Ridhiwan akizungunza na wakazi wa Kijiji cha Kwamduma, aliwahakikishia wananchi wa Kata ya Kibindu kuwa, shida ya maji inaenda kuwa historia, kwani shughuli za utendaji zinaendelea.

Alimshukuru Rais John Magufuli na serikali kwa hatua zinazochukuliwa kupata ufumbuzi wa shida ya maji katika kata hiyo na Jimbo zima la Chalinze.

"Serikali imejizatiti kuhakikisha maji yanawafikia wananchi wa Kibindu. Niwahakikishie kuwa miradi hii itakamilika kwa wakati na mapema ili wananchi wapate majisafi na salama," alisema.

Pia alieleza kuwa amefanya jitihada mbalimbali ikiwamo kuchimbwa kwa visima zaidi ya vinne katika vijiji vya kata hiyo ambavyo vimesaidia kidogo japo shida haijaisha.



Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA), Dk. Neema Kiure (kushoto), akikabidhi tuzo ya mshindi wa tatu wa uwakilishi bora wa hesabu katika kitengo cha benki kubwa zinazotolewa na NBAA kwa Kaimu Mkurugenzi wa Fedha wa Benki ya ABSA Tanzania, Bernard Tesha, katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali kuongeza kasi vita dhidi ya ukatili

Na Beatrice Shayo

SERIKALI imesema itaongeza kasi ya kupambana na kutokomeza aina zote za ukatili na unyanyasaji wa kijinsia, ikiwamo rushwa ya ngono kwa wanawake na watoto.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsi, Wazee na Watoto, Dk. John Jingu, wakati akifungua mkutano uliowakutanisha wanawake wa viongozi wa rika na ngazi zote kwa ajili ya kujadili jinsi ya kuongeza ushiriki wa wanawake wa rika zote katika nafasi ya uongozi na maamuzi ulioandaliwa na Mtandao wa Viongozi Wanawake wa Afrika (AWLN).

Alisema jambo hilo ni moja ya mkakati katika kutekeleza mpango kazi wa kitaifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto wa mwaka 2017/2018-2021/2022.

"Naelewa kuwa mkutano huu unafanyika katika kipindi cha kupinga siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia hivyo mtandao huu uendeleze jukumu la kutokomeza ukatili huo katika ngazi zote maana ukatili wa kijinsia ni changamoto katika kuwawezesha wanawake kushiriki katika nafasi za maamuzi na uongozi," alisema Dk. Jingu.

Alisema wizara yake itashirikiana na mtandao huo kuwaingiza wanawake wengi zaidi katika nafasi za maamuzi.

Kwa mujibu wa Dk. Jingu, jambo la muhimu ni kufanya kazi kwa kuzingatia sera, sheria, kanuni na vipaumbele vya serikali katika kufanikisha malengo waliyojiwekea na wajikite kufanya shughuli za maendeleo.

Aidha, alisema ili wanawake waweze kutoa mchango katika maendeleo ya nchi wanapaswa kuwa na maarifa sahihi, elimu na ndio maana serikali imesisitiza kila mtoto wa kitanzania ni lazima aende shule.

"Kutokana na sera ya elimu ni bure na sasa hivi serikali inatumia takribani Sh. bilioni 29 kila mwezi kwa ajili ya kugharamia elimu ya msingi na sekondari kwa watoto wetu kwa hiyo hakuna kisingizio kwa watoto wetu kutokwenda shule."

Aliongezea: "Lakini tunajua baadhi ya wazazi licha ya kuwapo kwa fursa hiyo wanawaoza watoto na baadhi ya wenzetu wenye tabia mbaya wanawafanyia ukatili watoto ikiwamo ubakaji na wengine kuwaleta huku mjini kufanya kazi za ndani kufanya hivyo ni kuwakosea watoto na taifa."

Dk. Jingu alisema kinamama wengi hasa vijijini wanapambana kujiendeleza kiuchumi na tatizo kubwa wanalokutana nalo ni mitaji, hivyo serikali kupitia mifuko ya halmashauri imetenga fedha kwa ajili ya wanawake ambazo ni asilimia nne ya mapato ya halmashauri ili wapate mitaji.

Aidha, alisema katika kuhakikisha ustawi wa maendeleo na jamii ya nchi serikali ni lazima ina hakikisha inabuni mikakati ya kuwawezesha wanawake wanapata fursa za kutosha kwenye nyanja za siasa na uchumi.

# Stanbic yapewa tuzo ya kutimiza mahitaji ya wateja

Na Elizabeth Zaya

BENKI ya Stanbic imetwaa tuzo ya benki bora kwa mwaka huu, kutokana na kutimiza mahitaji ya wateja wake na kuwa thabiti katika kipindi cha janga la ugonjwa wa corona.

Vigezo vingine ambavyo vimechangia benki hiyo kupata tuzo hiyo ni pamoja kuahirisha ulipaji wa mikopo ndani ya kipindi cha mlipuko wa ugonjwa huo na kuanzisha huduma maalum ya kuwasaidia wateja wake kuhimili katika kipindi cha COVID-19 iliyojulikana kama Afrika China Agency Proposition (ASAP).

Akizungumzia tuzo hiyo Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Stanbic, Kevin Wingfield, alisema, wamefanikiwa kupata tuzo hiyo kutokana na ushirikiano walioupata kutoka kwa wateja wao.

Alisema watahakikisha wanaendelea kujenga imani kwa wateja wao kama kauli mbiu yao ya mwaka huu inavyosema hususani katika kuongeza ubunifu na kuchagiza maendeleo ya nchi.

"Hii tuzo ni kielelezo cha juhudi zetu katika kuchangia maendeleo ya Tanzania na maendeleo ya shughuli zinazofanywa na wateja wetu hususani katika kuleta mabadiliko ya kiuchumi ukizingatia mwaka huu tunasherehekea miaka 25 ya uwapo wa Benki ya Stanbic nchini," aliongezea Wingfield.

"Benki ya Stanbic ni sehemu ya Standard Bank Group ambayo ni benki kubwa Afrika kwa umiliki wa mali na inapatikana katika nchi 20 barani kote."

Nipashe
# TESA
Jumanne Desemba 8, 2020
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI


Ukurasa 12

**Ulemavu wa akili ulivyotesa watoto darasani, nyumbani**


Ukurasa 13

HABARI MPYA:


Ukurasa 14

**DIT inavyosuka walimu kufundisha TEHAMA**

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

VIJANA VS AJIRA

# Mafunzo bila nyenzo, mitaji kujiajiri kunabakia kitendawili

KUKOSA mitaji ili kujiajiri kumekuwa kikwazo kipya kwa vijana wahitimu wa mafunzo ya ufundi stadi ambao licha ya kuwa na ujuzi, idadi kubwa imetumbukia kwenye shimo la wakosa ajira, wasaka kazi na wategemea kuajiriwa.

Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Shirika la Voluntary Service Overseas (VSO) la kanda ya ziwa, limekuja na mradi wa kuwasomesha vijana wa mazingira magumu, kusoma fani mbalimbali za ufundi na kuwapatia vifaa kuwawezesha kujiajiri na si kutegemea kuajiriwa.

Josam Katanga Mratibu wa VOS wa mradi wezeshi wa vijana kuinuka kiuchumi anasema mkoani Shinyanga vijana 200 wamesomeshwa fani mbalimbali katika Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA).

Anasema walifanya utafiti kubaini vijana wanaishi katika mazingira magumu walioshindwa kutimiza ndoto zao sababu ya hali ngumu ya uchumi wa kaya zao na kuwapata 200 kati yao 90 wanatoka Kahama na 110 Manispaa ya Shinyanga.



Mratibu wa mradi wa wezesha vijana kuinuka kiuchumi wa VSO, Josam Katanga, (wa pili kushoto), akikabidhi vifaa vya mapishi kwa wahitimu wa fani hiyo, wanaokwenda kujiajiri wenyewe. **PICHA: VSO**

**FANI WALIZOPITIA**

Katanga anataja upishi, saluni, mapambo, ushonaji mavazi, ufundi mabomba, umeme na kutengeneza pikipiki kuwa ni baadhi ya mambo waliyosomea na kwamba walipatiwa vifaa vya kuanzisha miradi, ili kujiajiri kulingana na walichojifunza. Wapo waliopata vyerehani, 'madraya' kwa salon, spana, majiko, ngazi, majora, vifaa vya ufundi na vya umeme.

"VOS tulibaini vijana wengi wanahitimu vyuo vya ufundi wanategemea kuajiriwa kutokana na ukosefu wa mitaji ya kujiajiri wenyewe na wale ambao hukosa ajira huishia mitaani na kuendelea kukabiliwa na ugumu wa maisha licha ya kuwa na ujuzi," anasema Katanga na kuongeza.

"Baada ya kulibaini hilo tatizo, shirika likaamua kuja na mpango wa kutoa vifaa kwa wahitimu ambao tunawafadhili mafunzo ya ufundi, ili wakajiajiri wenyewe na kuendesha maisha yao, bila ya kutegemea kutafuta kazi."

**KUGAWA VIFAA**

Ofisa Vijana Manispaa ya Shinyanga, Charles Ruchagula, anawataka waliohitimu mafunzo ya ufundi na kupata ujuzi, waache kubweteka na kusubiri kuajiriwa, bali wajiunge kwenye vikundi ili wapate mikopo ya vijana kwenye halmashauri.

"Vijana mliofadhiliwa mafunzo ya ufundi stadi na VSO, na kupewa vifaa vya kazi kujiajiri wenyewe, mkaitumie fursa hiyo vizuri, ili mjikwamue kimaisha na siyo kugawana vifaa hivyo, na kila mmoja kwenda na njia yake mtakuwa mmetuangusha sana," anasema Ruchagula.

"Natoa wito kwa wahitimu wengine kutoka vyuo mbalimbali vya ufundi nchini, mjiunge kwenye vikundi vya ujasiriamali na kujisajili, ili mkaombe mikopo ya vijana kwenye halmashauri na kupata mitaji ambayo itawasaidia kujiajiri wenyewe, pesa zipo nyingi na hazina riba," anaongeza Ofisa Vijana.

**KUFUATILIA MIENENDO**

Ofisa Maendeleo wa Kizumbi Manispaa ya Shinyanga, Wema Mashaka, anasema atafuatilia maendeleo ya vijana hao, mahali ambapo watafungua ofisi kwa ajili ya kujiajiri wenyewe, ili kujua maendeleo yao pamoja na changamoto ambazo zitawakabili na kuzitafutia ufumbuzi.

Anasema licha ya vijana hao kupewa vifaa kwa ajili ya kujiajiri wenyewe, bado wanahitaji msaada mkubwa wa kusimamiwa hadi wakomae kujitegemea na kuwa chini ya uangalizi wa maofisa maendeleo ya jamii.

"Mimi nitajitoa kusimamia maendeleo ya hawa vijana hadi wakomae na kujitegemea wenyewe, tukiwakabidhi vifaa hapa ili kwenda kujiajiri wenyewe bila ya usimamizi hawatofika mbali, sababu bado wanahitaji msaada wetu ukizingatia ndiyo wametoka chuoni na hawajui changamoto za kibiashara," anasema Mashaka.

Rashidi Ntahigiye, Msajili wa Wanafunzi Chuo cha VETA mkoani Shinyanga, ambaye, alikuwa mratibu wa mafunzo hayo ya kuwajengea uwezo vijana kiuchumi yaliyodhaminiwa na VSO, anasema vijana hao wameiva na wanao uwezo mkubwa wa kufanya kazi kulingana na fani walizosomea.

Anawataka vijana hao wanapoingia kwenye soko la kujiajiri wenyewe wajitume kufanya kazi, pamoja na kuwa wabunifu kwenye utengenezaji wa bidhaa zao, ikiwa soko hilo lina ushindani mkubwa, ili wafanikiwe kupata wateja wengi na kuinuka kiuchumi.

"Mnapotoka hapa chuoni na vifaa vyenu vya kwenda kujiajiri wenyewe, mkatafute vyumba vya kupanga kwa ajili ya kuanza kazi, na siyo mkaviuze vifaa hivi na kurudi mitaani kulandalanda na wakati njia ya mafanikio ya maisha mmeshapewa, kilichobaki na juhudi zenu tu," anasema Ntahigiye.

"Hii ni fursa kwenu, hakuna wahitimu katika chuo hiki ambao wanapewa vifaa kwa ajili ya kwenda kujiajiri wenyewe, wengi huo wanamaliza mafunzo na kwenda kutafuta ajira wenyewe, hivyo na wasihi sana muitumie fursa hii vizuri kwa mstakabali wa maisha yenu na taifa kwa ujumla ili muwe na mafanikio endelevu." Anaongeza.

Jumanne Desemba 8, 2020

ELIMU

NA MICHAEL ENEZA

# Ulemavu wa akili ulivyotesa watoto darasani, nyumbani



Fimbo silaha inayoendelea kuumiza wanafunzi na watoto nyumbani na shuleni. **PICHA: MTANDAO**

MOJA ya adhabu zilizoumiza watoto shule za msingi ni viboko, iwe ni kwa makosa ya kinidhamu au mengine kama usafi wa mwili, kutokujibu maswali kwa ufasaha na haraka darasani.

Waliosoma zamani watakumbuka ugumu wa kukariri orodha kuitaja kwa haraka, kwa mfano orodha ya saba, inaanza 7, 14, 21, 28, 35, ukipata kigugumizi hapo katikati fimbo inashuka, hata kama si kwa nguvu. Kulikuwa na adhabu za viboko za kuchelewa shule, kutofanya usafi vizuri na ukorofi.

Waliosoma miaka ya karibuni wapo katika hali tofauti kwa kiasi fulani, kwa vile elimu ni eneo ambako kanuni zinapitiwa na kufanyiwa marekebisho kila wakati kutoka kwa wadau kwa upande mmoja na miongozo ya kimataifa kwa upande mwingine.

Mara nyingine mabadilimo yanaanzia katika ngazi ya wizara inayoona kuna haja ya kurekebisha mambo yalivyo katika eneo hili au lile. Hata hivyo, adhabu ya viboko imeendelea kutingisha jamii, kwa watoto na hata walimu.

Ukiangalia unakuta kuwa hapakuwa na njia rahisi au ya wazi ya kujua sababu za mtoto kushindwa kukariri orodha na watoto wanachukuliwa kana kwamba wana uwezo sawa wa kuelewa na kujibu ni kama suala la nidhamu. Nje ya hapo, ingebidi mwalimu atafute sababu mtoto anashindwa kujibu swali au kukariri orodha hii au ile na siyo kumwadhibu kana kwamba amefanya kosa la kukusudia.

Ni mazingira ambayo yaliwakosesha watoto raha, kama ilivyokuwa 'kodi ya kichwa' kwa watu wazima vijijini ikiumiza wanaume au wakuu wa nyumba, waliolazimika kujificha wasikamatwe na kudaiwa.

Mojawapo ya vielelezo vya kushindwa kwa mwanafunzi kuelewa darasani na kujibu maswali kwa ufasaha ni wenye mtindio wa ubongo, ambao si ulemavu wa wazi kama wa uziwi au upofu.

Ni miaka ya karibuni ndipo imeanza kufahamika nini hasa kiwango cha ulemavu wa akili (kudumaa) kwa watoto wanaofikia umri wa kuanza shule, na athari zake katika kumudu masomo.

Upana wa tatizo la wenye mtindio wa ubongo au udumavu wa akili ni mkubwa, kwani hugusa idadi kubwa ya watoto.

Ingebidi kufanya utafiti kiasi fulani kujua ni kwa kiasi gani suala hilo limefanyiwa kazi wizarani na miongozo kutolewa kuhusu mbinu za kufundishia zinazotumika, lakini inawezekana mbinu hii ya masomo ya ziada ndiyo jawabu, badala ya 'kupiga tu.' Jambo ambalo si rahisi kusema ni kama kuanzishwa kwa masomo ya ziada ni kujazia upunguzu wa kuelewa watoto au kunaendana vile vile na mikakati ya kufundisha kwa udhaifu, mojawapo ya sababu ikiwa ni hali ya watoto kutokuelewa na kumkatisha mwalimu tamaa.

Watoto wanapokuwa wengi darasani kuliko idadi inayokubalika kimataifa na hata kwa kanuni rasmi hapa nchini halafu kuna waliodumaa ina kuwa kazi ngumu.

Baadhi ya watoto waliokuwa na familia ambako baba ni mwalimu walikuwa na hali ngumu zaidi, kwani shuleni akikosea anachapwa, akirudi nyumbani kunakuwa na 'tuisheni' ambako anatandikwa pia.

Si rahisi kujua kama watoto waliokuwa katika mazingira kama hayo wangeweza kusoma vyema na kuelewa hadi darasa la saba baada ya darasa la nane kufutwa.

Nafasi za sekondari zilikuwa chache lakini za ufundi au 'ujuzi' wa aina nyingine zilipatikana hata sasa zipo.

Jambo ambalo si rahisi kusema ni kama nyakati hizo viwango vya utapiamlo ambavyo ni kiini cha ulemavu wa ubongo vilikuwa kama sasa na kama theluthi moja ya watoto imekuwa na ugumu huo wa kuelewa tangu uhuru, au hilo ni tatizo ambalo lilizuka baadaye.

> Baadhi ya watoto waliokuwa na familia ambako baba ni mwalimu walikuwa na hali ngumu zaidi, kwani shuleni akikosea anachapwa, akirudi nyumbani kunakuwa na 'tuisheni' ambako anatandikwa pia.

Sababu mojawapo ya sintofahamu hiyo ni kuwa utapiamlo wa watoto umeendana na uharibifu wa mazingira maeneo ya vijijini, wakati mijini hali itakuwa ni afadhali. Kuna njia nyingi zaidi za vipato na kuinua lishe kwa watoto, licha ya taabu nyingi.

Pamoja na mabadiliko ambayo yamefanyika kuhusiana na kutumika kwa fimbo kama nyendo ya kuendesha darasa kila uchao, kuna uwezekano mkubwa wa mapungufu ya uelewa wa sababu za watoto kutokufuatilia vyema wanachofundishwa.

Si rahisi kumwangalia mtoto machoni ujue kuwa ana mtindio wa ubongo na badala yake mwalimu ataona kitu kingine, kuwa kila wakati anacheza, siyo kusoma, au kama ni miaka ya karibuni au karne hii, hahudhurii 'tuisheni,' hivyo anachapwa ili mzazi atoe fedha ya 'tuisheni'.

Mvutano wa shule, walimu na wazazi ulisababisha watoto kuumia.

Siyo rahisi kusema kama matumizi hayo ya adhabu yaliwasukuma watoto kusoma kwa bidii zaidi au kuhudhuria shule vyema zaidi, ingawa ni kweli watoto wadogo wasipohofia chochote wanaweza kubaki katika mchezo tu wasifanye lolote la maana.

Tatizo ni pale uelewa huo unapoondoa udadisi halisi wa hali ya mtoto jambo ambalo haliwezi kufanyika katika ngazi ya kila shule na kila mwalimu ila kufanyiwa kazi wizarani na miongozo kufikishwa shuleni.

Badala ya viboko, inatangulia kwanza tathmini ya viwango halisi vya uwezo wa mtoto kuelewa na ikibidi madarasa yatenganishwe.

Ufundishaji unahitaji kuwa na darasa lenye watoto wenye viwango vinavyokaribiana vya uelewa ili mwalimu asichoshwe na wale wanaokwenda polepole.

Ni eneo ambalo siyo rahisi wakuu wa shule kulifanyia kazi kwani hawawezi kugawa madarasa kwa makundi kadhaa, ili kuwa na mtiririko tofauti wa ufundishaji kulingana na uelewa.

Kwa maana hiyo wanabaki na madarasa hayo na mbinu hizo za kufundishia, ikiwa ni pamoja na viboko na tuisheni. Kwa hali hiyo watoto wa familia maskini wanapata utapiamlo, hivyo kuwa waathirika zaidi wa udumavu na viboko darasani.

TEKNOLOJIA
**NA GAUDENSIA MNGUMI**

# HABARI MPYA:
## ■Hakuna kuzeeka, DNA kukarabatiwa
## ■Pesa mtandaoni kuua sarafu, noti




Sarafu mtandao 'bit coin' inayokuja kwa kasi ya kubadilisha sura ya matumizi ya pesa duniani.

TEKNOLOJIA ni suala ambalo halikwepeki na mwaka unavyokwisha kuna mengi yanayozungumzwa kuhusu ugunduzi na utafiti mpya uliofanyika miaka ya karibuni na kuzaa matunda 2020.

Kwa Afrika, bara linaloendelea kiuchumi kuna mengi yamefanywa, aidha sehemu nyingine nazo kuna ripoti za kusisimua kwenye ugunduzi na mafanikio kwenye tiba, mawasiliano na uchumi.

Mwaka huu, kampuni ya 'mPedigree', iliyoanzishwa mwaka 2007 na mjasiriamali wa teknolojia wa Ghana, Bright Simons, inasifika kwa kufanya makuu, kwa kutengeneza dawa ya kudhibiti bidhaa feki.

Imetengeneza alama ya utambulisho au 'code' ambayo mteja wakati wowote anaituma kiwandani kwa wazalishaji kuuliza iwapo bidhaa aliyonunua ni feki au halisi.

'Code' au utambulisho huo unatumiwa sehemu kubwa ya Afrika na umewaunganisha wateja na kamapuni kubwa za dawa duniani mbinu ambayo imedhibiti dawa feki na bandia. Teknolojia hiyo imerahisha pia kufuatilia na kujua chanzo cha bidhaa ziwe vyakula, mazao ya kilimo na hata vifaa vya kielektroniki.

KUKOMESHA MOTO

Kampuni ya LUMKAN ya Afrika Kusini ni moja ya wadau walifanya maajabu mwaka huu eneo la kudhibiti moto na kuweka mambo sawa hasa kuhakikisha usalama wa watu na mali zao unaotishiwa na moto unaotokana na umeme, milipuko ya gesi na hata vifaa.

Kampuni hiyo imeunda mfumo wa tahadhari unaotoa maonyo mapema iwapo moto utatokea kwenye makazi ya watu hasa mijini na vitongoji vya nchi. Vifaa vya LUMKAN vilivyoundwa kutambua mabadiliko ya hali ya joto hasa kuhisi moto na wala si uwepo wa moshi vimesambazwa karibu nyumba 40,000 ambazo sasa zina ulinzi mahususi wa tahadhari ya moto.

**UZEE KUDHIBITIWA**

Tiba ya kudhibiti uzee au 'anti-aging drugs' mwaka 2020 unashuhudia watafiti wakikaribia kupata dawa ya kuzuia kuzeeka na wakati wowote dawa hizo ziwe vidonge au sindano na hata za kunywa zitaanza kufurika sokoni.

Ni habari njema kwani utakuwa ndiyo mwanzo wa kudhibiti au kupunguzwa nguvu magonjwa yasiyoambukizwa kama saratani, usahaulifu, kiharusi, moyo na kisukari ambayo yanaweza kuwa na uhusiano na umri mkubwa au uzee.

Tiba hizo zitakuwa zinapambana na mchakato wa kuzeeka na kwamba majaribio mengi yameanza kuonyesha mafanikio kwa binadamu waliozitumia baada ya majaribio kadhaa.

**KUBANA WADUKUZI**

Mwaka huu umekuwa wa mafanikio katika kuwabana wadukuzi hasa wa mawasiliano mitandaoni na taarifa za siri. Hii ni kutokana na ugunduzi wa mtandao 'usiodukulika' au 'Unhackable Internet'.

Ni mafanikio kwa sababu mawasiliano ya intaneti yalikuwa hatarini kwa vile kila jambo lingeweza kudukuliwa na taarifa kuwekwa hadharani bila kujali usalama wa wateja au taifa.

Wadukuzi miaka ya karibu walifanikiwa kuingia kwenye mitandao iwe ya intaneti, simu na webu na kupata taarifa muhimu za kiserikali, za benki, mashirika, ujasusi, mawasiliano ya simu na kwa ujumla ilikuwa ni changamoto kiusalama.

Wataalamu wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHEMA) wanajitahidi mchana na usiku kukamilisha kutengeneza intaneti isiyodukuliwa na ambayo si rahisi wadukuzi kuihujumu.

Mojawapo wa wadau wakuu wanaotengeneza intaneti hiyo ni Chuo Kikuu cha Teknolojia cha Delft (Delft University of Technology) kilichoko Uholanzi.

**INTANETI POPOTE**

Leo hii wengi hawajaweza kufurahi kutumia mtandao kuangalia picha, kusoma ujumbe, kutuma kwa kuwa wana hofu ya bando (kifurushi).

Hayo yanaelekea ukingoni kwa vile dunia ambayo inategemea teknolojia ya Wi-Fi husomwa 'waifai' kujiunganisha na huduma za intaneti inaanza kupatiwa mbadala.

Wi-Fi inatumia mawimbi yanayounganishwa bila waya au nyaya au 'wireless', lakini haijasambaa vya kutosha na kufikia watumiaji wengi.

Ndiyo maana dunia sasa inaanza kutumia teknolojia iitwayo 'satellite mega-constellations' inayolenga kufikisha masafa (signals) ya intaneti yenye kasi kubwa kila kona ya dunia, kila taifa, kijiji na hata mtaa. Inaelezwa kuwa teknolojia ya 'satellite mega-constellations' itakuwa ni mbadala wa masafa ya 'spotty Wi-Fi', hivyo intaneti popote

**PESA MTANDAONI**

Matumizi ya pesa ya mtandao au 'digital money' yanavyoshika kasi, ndivyo pesa za makaratasi na sarafu zinavyoelekea kuwekwa pembeni. Si mbali habari za kutembea na noti kama za Sh. 10,000, 5,000 au 2,000 na Sh. 200 yatabakia kuwa historia japo pengine kwa mataifa yanayoendelea kujenga uchumi wake hasa ya Afrika huenda ikachukua muda kubadilika.

Pesa ya kidijitali inavyoendelea kutumiwa kuna athari kwenye masuala ya fedha ambayo huenda yakapunguza usiri kwa vile kila kitu kitakuwa kwenye mtandao wa kielektroniki hasa kwenye kununua na kuuza na kutunza fedha kwenye akaunti zenye kutumia 'crypto currencies'.

**TIBA BINAFSI**

Tiba iliyopewa jina la 'hyper-personalized medicine' maalumu kwa ajili ya mtu mwenye matatizo yake binafsi hasa magonjwa yanayotokana na kuvuruga kwa nasaba au 'genetic mutation' kwa mtu mmoja siyo tatizo tena.

Ni matibabu yanayotolewa kwa ajili ya maradhi ambayo hapo awali yalikuwa hayatibiki haya ni kama saratani, kisukari na kuharusi.

Ni dawa ambazo zimeanza kutumiwa kutibu wakati huu kwa kuangalia jene za mgonjwa zinazoathiriwa na kasoro kwenye DNA na kinachofanyika sasa ni kukarabnati jeni 'genetic fix' ili kuwa na nasaba zisizo na kasoro.

Ugunduzi huu unatokana na tiba ya Mila Makovec, binti aliyekuwa na maradhi hatarishi yaliyotokana na kuvurugika kwa DNA au nasaba na kuwalazimisha wataalamu kutengeneza dawa mahsusi kwa ajili yake na zikapewa jina la milasen zikarejea jina lake.

Dawa hizo japo hazikumponyesha zilipunguza changamoto za kifafa, aliweza kusimama na kutembea japo kwa kusaidiwa jambo ambalo hakulifanya hapo mwanzoni.

**MITANDAO**



Mawimbi ya Wi-Fi yanayounganishwa bila nyaya yamepata mbadala ambao utawezesha kufikisha intaneti karibu duniani kote. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

TEKNOLOJIA
**NA SABATO KASIKA**

# DIT inavyosuka walimu kufundisha TEHAMA

## Umeme wabaki kikwazo shule vijijini



Wanafunzi wakitumia kompyuta kupakua taarifa mbalimbali kwenye mtandao. **PICHA: MWANDISHI WETU**

WALIMU 602 wa shule za msingi na sekondari, wanapikwa katika mafunzo ya umahiri wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) yanayowapa mbinu za kuboresha somo hilo madarasani.

Lakini, ili wasiishie hapo wanajengwa kukarabati vifaa vya TEHAMA kama kompyuta na simu ili vidumu.

Aidha, wanafunzwa kuvitunza ili visiharibike kila wakati, ndivyo anavyosema Mkuu wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Profesa Prescedius Ndomba, wakati wa uzinduzi wa mafunzo hayo.

Walimu hao 602 wa shule za msingi na sekondari kutoka bara na visiwani, wanafunzwa kuwa na umahiri katika TEHAMA ili kuendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Anasema baadhi ya vifaa hivyo vya TEHAMA, wanavyojifunza jinsi ya kuvikarabati na uwezo wa kuvitunza ili visharibike na kuunganisha mawasiliano ni kompyuta za mezani na mpakato (laptop).

Mkuu wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam anafafanua hayo wakati wa uzinduzi wa mafunzo hayo hivi karibuni na kusema DIT ndiyo inayotoa mafunzo hayo ya kimkakati, yanayogharamiwa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), chini ya Kituo cha Umahiri wa TEHAMA Taifa (ITCoEICT).

"Mafunzo hayo ni ya muhimu ili kusaidia walimu kufanya ukarabati mdogo kwa vifaa hivyo, DIT tunatoa wawezeshaji, vifaa vyenyewe na miundombinu mingine ya kufanikisha mafunzo," Prof. Ndomba anasema.

Anafafanua kuwa yanawaimarisha walimu kufundisha wanafunzi somo la TEHAMA na hata kompyuta inapopata tatizo dogo, inakuwa rahisi kwao kuikarabati na siyo kuachana nayo na kutafuta nyingine.

"Ninaishukuru serikali kwa kutoa Sh. milioni 37 kwa Kituo cha Umahiri cha TEHAMA cha Taifa, ili kuendelea kuimarisha na kuboresha uendeshaji wake ikiwa ni njia mojawapo ya kuboresha TEHAMA shuleni," anasema.

Aidha, anafafanua kuwa, kwa mwanafunzi aliyefundishwa TEHAMA, inamuwia rahisi kupakua vitabu vya masomo katika kompyuta au laptop kwa ajili ya maendeleo yake kielimu.

"Kwa hiyo mwalimu wa TEHAMA atahitaji kuwa na ujuzi na maarifa yeye mwenyewe ikiwamo kuunganisha mawasiliano ya mtandao ambayo atayepeleka kwa mwanafunzi wake ili ajue kutumia kompyuta au laptop kupakua masomo," anasema.

### UKARABATI VIFAA

Mkurugenzi wa Kituo cha Umahiri cha TEHAMA, Dk. Aliila Kenedy, anasema, mwalimu kujua jinsi ya kukarabati vifaa vya TEHAMA hasa kompyuta na uwezo wa kuvitunza ni muhimu kuhakikisha mafanikio endelevu.

"Mwalimu hatakiwi kujua kufundisha tu bali pia ajue matengenezo madogo ya kompyuta, kwani hatua hiyo inasaidia hata kuwa na matunzo ya kompyuta," anasema Dk. Kenedy.

> "Mfuko unatekeleza miradi mbalimbali ya kutoa huduma ya mawasiliano nchini, na shule za umma takriban 700 zimeshapelekewa vifaa vya TEHAMA hasa kompyuta kwa ajili ya walimu," anasema Mashiba.

Mkurugenzi wa Mfuko wa UCSAF, Justina Mashiba, anasema, kutokana na jitihada mbalimbali zinazoendelea kufanywa na mfuko huo, asilimia 94 ya Watanzania wanapata huduma ya mawasiliano.

"Mfuko unatekeleza miradi mbalimbali ya kutoa huduma ya mawasiliano nchini, na shule za umma takriban 700 zimeshapelekewa vifaa vya TEHAMA hasa kompyuta kwa ajili ya walimu," anasema Mashiba.

Anafafanua kuwa walimu 1, 656, wamepata mafunzo, na kwamba mwaka huu wengine 602 wanaendelea na kupata mafunzo, yanayozingatia utekelezaji wa sera ya elimu ya mwaka 2014 ikiwa ni pamoja na kuweka mkazo katika TEHAMA ili kuchangia maendeleo ya nchi.

### KUUNDIWA MTAALA

TEHAMA ilianzishwa katika mtaala mpya wa elimu ya msingi na wizara husika mwaka 2005, kwa lengo la kumpa mwanafunzi maarifa na stadi za matumizi ya habari, vyombo vya mawasiliano na maktaba.

Tangu kuanzishwa kwa somo hilo, wadau mbalimbali wa elimu, wanaendelea kutoa mafunzo kwa walimu kwa ajili ya kuwaongozea wanafunzi uwelewa wa somo hilo, ili iwe rahisi katika ufundishaji na ujifunzaji shuleni.

Miongoni mwa mafunzo hayo ni yale umahiri ya TEHAMA yanayoendelea yakishirikisha walimu 602 wa shule za msingi na sekondari kutoka bara na visiwani, ingawa yamo mengi tu ambayo yamewahi kufanyika.

Hayo yanafanyika kutokana na ukweli kwamba, dunia ya sasa ya utandawazi, imesababisha kuzagaa kwa matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, hususan kompyuta na vifaa vyake katika nchi mbalimbali.

Tanzania nayo haijabaki nyuma, kwa kuwa baadhi ya shule za msingi na sekondari zinafundisha somo la TEHAMA, tangu lilipoingizwa katika mtaala mwaka 2005, huku mafunzo yakiendelea kutolewa kwa walimu na wanafunzi.

### SHULE ZA VIJIJINI


Katibu Mkuu wa Chama cha Wamiliki na Mameneja wa Shule na Vyuo Binafsi (TAMONGSCO), Benjamin Nkonya, anasema, kuna haja kwa serikali kufanya mabadiliko makubwa kwenye TEHAMA kwa shule za vijijini.

Anasema, shule za binafsi zilizopo vijijini zina umeme wa sola, lakini za serikali hazina, hivyo somo hilo hufunzwa kinadharia tu, hali ambayo unaweza kuwafanya wanafunzi wasiambulie chochote.

"Huwezi kuchora kompyuta ubaoni na kuanza kuwafundisha wanafunzi kwani ni vigumu kuelewa kuiona ilivyo, kwa hiyo nieleweke kuwa kufanya hivyo ni sawa na kuigiza," anasema Nkonya.

Anasema, kutokana na mabadiliko ya teknolojia ya mawasiliano duniani kuathiri nyanja mbalimbali za maisha, TEHAMA inatakiwa kwa wanafunzi wote wa shule za mjini na vijijini.

"Kama serikali haina uwezo wa kupeleka umeme wa TANESCO katika shule zake zote za vijijini, basi iweke hata wa sola, ili iwe rahisi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo hilo kuliko ilivyo sasa," anasema.



# Askofu ashauri mawaziri kuombewa

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

ASKOFU wa kanisa la International Evangelism Sinai Ipagala Dodoma, Sylvester Thadey, amewataka Watanzania kuliombea baraza jipya la mawaziri lililoteuliwa na Rais John Magufuli, ili wafanye kazi kwa malengo ya kuiletea nchi maendeleo bila kujali itikadi za chama, dini, rangi au kabila.

Thadey, aliyasema hayo juzi jijini Dodoma alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu Baraza jipya la Mawaziri lilitangazwa mwishoni mwa wiki.

Alisema Rais Magufuli tayari ameteua Baraza la Mawaziri pamoja na manaibu wake, hivyo Watanzania wanatakiwa kuwaombea ili kufanya kazi kwa uaminifu, uzalendo na kwa maadili ambayo yatakayowezesha Taifa kuwa na maendeleo ya kiuchumi.

Alisema kuwaacha peke yao mawaziri na manaibu wao bila msaada wa maombi, wanaweza kuwa na wakati mgumu, hivyo Watanzania kama ilivyo destuli wanatakiwa kuwaombea.

Aidha, aliwaomba Wakristo kujijengea tabia ya kumtegemea Mungu wanapohitaji kujiletea maendeleo yao ya kiroho na kiuchumi badala ya kutegemea ufadhili kutoka nje.

Alisema waumini ni muhimu wakajijengea utamaduni wa kutumia rasilimali zao, badala ya kuelekeza kuomba misaada kutoka kwa wafadhili wa nje.

"Hata hao wafadhili pia wanamtegemea Mungu kwenye mahitaji yao wanayoyahitaji, hivyo hata sisi pia tunahitaji kumtegemea huyo Mungu kwa ajili ya maendeleo yetu," alisema.

# Serikali yaita wawekezaji sekta ya elimu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Josephat Maganga, amewataka wawekezaji kujitokeza kwa wingi kuja kuwekeza kwenye sekta ya elimu jijini Dodoma, kutoka na mahitaji makubwa ya shule za kisasa na ubora wa kimataifa uliopo.

Maganga, aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na wazazi na viongozi mbalimbali katika sekta ya elimu kwenye mahafali ya kwanza ya shule ya awali na msingi ya Ellen White, iliyopo Nzuguni jijini Dodoma.

Alisema, kutokana na serikali kuhamia Dodoma, hivi sasa mahitaji ya shule yameongezeka kutokana na idadi kuwa ya watu walipo.

"Tunawakaribisha sana wawekezaji, maeneo bado yapo mengi kwa ajili ya kufanya uwekezaji, hivyo niwaombe waje kwa wingi ili wawekeze katika sekta ya elimu," alisema Mganga.

Aidha, alisema katika jitihada za kukuza elimu katika Wilaya ya Dodoma mikakati iliyopo ni kujenga madarasa, nyumba za walimu, mabweni pamoja na kuboresha miundombinu mingine ya elimu.

"Pamoja na jitihada hizo, lakini niwatake walimu, waratibu elimu kata pamoja na maofisa elimu kila mmoja atimize wajibu wake, ili kuhakikisha kuwa Jiji la Dodoma elimu inakuwa," alisema Maganga.

Mwenyeki wa Kamati ya shule hiyo, Mchungaji David Mbaga, alisema lengo la shule hiyo ni kuhakikisha kuwa inatoa elimu bora ambayo itawawezesha wahitimu kuwa na uwezo wa kujitegemea.

"Tunataka kutoa elimu bora ambayo watoto wakitoka hapa wawe na uwezo wa kujitegemea na siyo kuwa tegemezi kwa kuwajengea maarifa, lakini tunaiomba serikali kuwashika mkono wawekezaji wanaojitokeza katika sekta ya elimu, ili ufike wakati kusiwe na Mtanzania anayetamani kupeleka nje ya nchi mtoto wake kwenda kusoma," alieleza Mchungaji Mbaga.

Mkurugenzi wa shule hiyo, Simon Ikwabe, alisema kuwa malengo ya shule hiyo ni kuwa ya mfano nchini katika utoaji wa elimu bora inayowawezesha wahitimu kuweza kujitegemea.

"Haya ni mahafali yetu ya kwanza kwa darasa la saba tumekuwa wa kwanza katika Jiji la Dodoma na wa pili kimkoa hivyo lengo letu ni mwakani kuwa kwenye kumi bora za kitaifa," alisema.

Hata hivyo, alisema kuwa wanalenga kuwekeza katika kiwango cha juu, ili elimu inayotolewa katika shule hiyo iwanufaishe watoto wanaomaliza darasa la saba na kuwa wa mfano.



Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Josephat Maganga, akifafanua jambo wakati akitoa hotuba yake kwenye mahafali ya Shule ya Awali na Msingi ya Ellen White iliyopo Nzuguni, jijini Dodoma, jana, kulia ni Mkurugenzi wa shule hiyo, Simon Ikwabe. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Mkakati waja kuwawezesha vijana, wanawake kilimo bustani

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeandaa mkakati wa vijana na wanawake wanaofanya kilimo cha mazao ya bustani kujiunga katika vikundi na vyama vya ushirika.

Lengo la mkakati huo ni kukidhi viwango vya ushindani na manunuzi katika soko la kimataifa.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mazao Wizara ya Kilimo, Nyasebwa Chimago, alisema hayo katika mkutano na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki jijiji Dodoma.

Chimago alisema wizara inafanya hivyo kutekeleza mkakati huo, ili kutimiza agizo la Rais John Magufuli la kuimarisha sekta ya kilimo cha mazao ya bustani kwa lengo la kufikia viwango vinavyohitajika kimataifa.

Alisema wakulima hao wakijiunga katika vikundi na vyama, itawasaidia bidhaa zao kukidhi kiwango kinachohitajika katika soko, ubora pamoja na ushindani wa kibiashara katika soko la nje.

"Wizara tunatekeleza agizo la Rais Magufuli ambaye alizitaka Wizara ya Kilimo, Biashara, Mambo ya Nje, mabalozi na sekta binafsi kujipanga kutafuta masoko na kusaini makubaliano yatakayoinufaisha nchi," alisema Chimago.

Chimago alisema kama ilivyoainishwa awali, serikali imekusudia kununua ndege ya kusafirisha mizigo ili kurahisisha usafirishaji wa mazao ya kilimo cha bustani, mifugo, minofu ya samaki na nyama, hivyo wizara inapaswa kuhakikisha sekta hiyo ndogo ya kilimo inaimarika katika uzalishaji.

Akitolea mfano wa mazao ya maharage madogo yanayolimwa mkoani Iringa, alisema kwa wiki katika soko la Uingereza zinahitajika kontena 20, lakini mkulima mmoja anakuwa na kontena tano, hivyo wakulima wakijiunga katika vikundi au vyama vya ushirika itakuwa rahisi wao kufikia kiwango hicho.

Kutokana hali hiyo, ndio maana wizara imekuwa ikisisitiza wakulima kuhakikisha wanajiunga katika vikundi au vyama vya ushirika ambavyo vitawasaidia kupiga hatua katika kilimo wanachofanya ili kilete matokeo chanya kwao na kwa taifa.

Mkurugenzi huyo alisisitiza kuwa endapo wengi wa wakulima wa mazao hayo wataungana, watapata fursa ya kubadilisha mawazo ya namna ya kuendesha kilimo hicho ikiwamo kujadili kero mbalimbali za kibiashara.

Katika hatua nyingine Katibu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, alisema Tanzania inashika nafasi ya 20 katika uzalishaji wa mazao ya bustani ambayo ni miongoni mwa sekta ndogo ya kilimo.

Kusaya alisema mauzo ya mazao ya bustani kwenda nje ya nchi yameongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 412 kwa mwaka 2015 hadi kufikia Dola za Marekani milioni 779 kwa mwaka 2015.

HABARI MBEYA

# Mamia wakosa makazi kisa nyumba kuezuliwa

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

ZAIDI ya kaya 108 za vijiji vitatu vya Kata ya Ipinda katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, hazina mahali pa kuishi baada ya nyumba zao kuezuliwa na upepo mkali ambao pia uliezua Shule ya Sekondari Ipinda.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maafa ya Wilaya ya Kyela, Amos Kayembele, alisema upepo huo ulifanya uharibifu huo wiki iliyopita, hivyo baadhi ya wananchi kulazimika kuhifadhiwa na majirani, huku baadhi wakiendelea kuzikarabati wakati wakiendelea kuishi humo.

Alivitaja vijiji vilivyokumbwa na upepo huo ni Kafundo kaya 35, Ikulu kaya 16 na Ipinda kaya 57 na kwamba katika Shule ya Sekondari Ipinda madarasa, vyoo vya walimu pamoja na maktaba viliezuliwa.

Alisema wanaendelea kufanya jitihada za kuirejesha baadhi ya miundombinu ya umma hasa shule, ili wanafunzi waendelee na masomo, huku akiwataka wananchi kuendelea kukarabati nyumba zao na wale ambao walinusurika waendelee kuwahifadhi wenzao.

"Tunamshukuru Mungu hakuna hata mmoja aliyepoteza maisha wala kujeruhiwa kwenye tukio hili zaidi ya nyumba zao kuezuliwa paa na zingine kubomoka kabisa," alisema Kayembele.

Kaimu Ofisa Mtendaji wa Kata ya Ipinda, Edward Mohamed, alisema wameanza kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwamo wawekezaji wa kilimo cha kakao kwa ajili ya kukarabati Shule ya Sekondari Ipinda ili wanafunzi waendelee kusoma.


Alisema wanafunzi ambao madarasa yao yaliezuliwa wamehamishiwa kwenye vyumba vilivyokuwa vinatumika kama maabara, huku akieleza kuwa ili kuirejesha miundombinu hiyo zinahitajika Sh. 8,000,000.

Alisema baadhi ya wadau wameahidi kujitolea saruji kwa ajili ya ukarabati, huku wakiweka masharti kwamba watapeleka vifaa hivyo baada ya kuhakikishiwa kuwa mafundi wameshapatikana ili wakitoa vifaa hivyo vianze kufanya kazi.

"Tunataka baada ya wiki tatu zijazo madarasa haya yawe yamekamilika na wanafunzi waanze kusoma, kuna baadhi ya majengo tutatakiwa kuyabomoa mpaka usawa fulani, ili tuanze kujenga, lakini upande mmoja wa ofisi ya walimu tunatakiwa kuanza upya," alisema Mohamed.

Mbunge wa Kyela, Ally Jumbe, alifanya ziara juzi katika vijiji vyote vilivyokumbwa na tatizo hilo kwa ajili ya kujionea uharibifu na kutoa misaada mbalimbali kwa waathirika.

Baada ya kujionea madhara hayo, alitoa Sh. 4,000,000 kwa ajili ya kuwalipa mafundi watakaokarabati shule pamoja na kuahidi kuwachangia wananchi waliopata madhara.



Mbunge wa Jimbo la Lupa, Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, Masache Kasaka (kushoto), Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Mbeya ambaye ni Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi (kulia) na Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Saimon (katikati) wakikagua mradi wa ujenzi wa barabara ya Chunya – Makongolosi inayojengwa kwa kiwango cha lami. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mbeya-WSSA yaomba mil.75/- kumaliza kero ya maji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA), imeiomba Serikali Kuu kuiwezesha Sh. nilioni 75 ambazo zinahitajika kwa ajili ya kujenga mradi wa maji wa Mto Kiwira ambao ukikamilika utamaliza tatizo la maji mkoani humo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka hiyo, Edna Mwaigomole, alitoa ombi hilo wakati wa ziara ya Mbunge wa Mbeya Mjini ambaye ni Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, kwenye miradi mbalimbali ya maji katika jiji hilo.

Mwaigomole alisema endapo mradi huo utakamilika, utamaliza tatizo la maji pamoja na kuwezesha shughuli za maendeleo kuimarika zikiwamo shughuli za viwanda ambazo alisema zinahitaji maji mengi.

Alisema tathimini ya mradi huo imeshakamilika na sasa kilichobakia ni kutafuta fedha ambazo zitatumika kuujenga mradi huo kutoka kwenye chanzo mpaka kuyafikisha Mbeya Mjini na kusambaza kwenye wilaya mbalimbali ambazo zina uhitaji.

"Jiji la Mbeya ndiye 'center' (kitovu) cha uchumi wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini hivyo shughuli nyingi zinazohitaji maji zinafanyika hapa, lakini pia hata ongezeko la watu ni kubwa sana, kwa hiyo huu mradi kwa sasa unahitajika sana," alisema Mwaigomole na kuongeza:

"Tunaiomba Serikali Kuu itusaidie kwa sababu fedha zinazohitajika ni nyingi kiasi kwamba tukitaka kuutekeleza sisi wenyewe itatuchukua muda mrefu kuukamilisha."

Mkurugenzi Mtendaji wa Mbeya-WSSA, Mhandisi Ndele Mengo, alisema mradi huo ukikamilika utalifanya jiji hilo kuwa na asilimia 100 za upatikanaji wa maji pamoja na kupunguza tatizo hilo katika mkoa jirani wa Songwe.

Alisema hata baadhi ya wilaya za mkoa huo zikiwamo Chunya, Mbarali na Rungwe zitanufaika kwa kusambaziwa huduma hiyo muhimu kwa maisha ya binadamu na viumbe wengine.

Mhandisi Mengo alisema mradi huo utakuwa na uwezo wa kuzalisha lita 100,000 za maji kwa siku na kwamba mahitaji ya maji kwa Jiji hilo ni lita 70,000 kwa siku kulingana na idadi ya watu waliopo.

Alisema kwa sasa jiji hilo linakabiliwa na upungufu wa lita 30,000 za maji kwa siku kutokana na kuwa na uwezo wa kuzalisha lita 40,000 kwa siku kutoka kwenye vyanzo vyote vilivyopo vikiwamo visima.

"Matarajio yetu ni kwamba lita 30,000 za ziada ambazo tutazalisha tutazigawa kwa wenzetu wa wilaya za Chunya, Mbarali na Mkoa wa Songwe ambao pia unakabiliwa na tatizo la upungufu wa maji," alisema Mengo.

# Ombi 'ma-miss' utalii kutangaza vivutio vya utalii

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imeombwa kuwatumia 'mamiss' utalii 40 kutoka katika mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara na Visiwani walioko mkoani humo kutangaza vivutio vya utalii vilivyomo ili kuinua sekta hiyo muhimu kiuchumi.

Mdau wa Maendeleo wa Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela, alitoa ombi hilo juzi baada ya walimbwende hao kutembelea shule ya Msingi ya Mchepuo wa Kiingereza ya Paradise Mission pamoja na kufanya shughuli mbalimbali za kijamii katika Mji wa Mbalizi.

Mwaselela alisema Serikali ya Mkoa inaweza kuwatembeza warembo hao kwenye maeneo hayo ya vivutio ili wakavitangaze kwenye mikoa yao waliyotokea na hivyo kuvutia watalii wa ndani na nje ya nchi.

Alisema aliwaleta warembo hao mkoani Mbeya kwa ajili ya kufanya nao matangazo ya shule yake, lakini akaona ni vema na serikali ikawatumia kwenye shughuli hizo za kiuchumi.

"Wameshachaguliwa kwenye mikoa yao kwamba wanafaa kuwa mamiss utalii, sasa wamekuja Mbeya kwa ajili ya Paradise Mission, nina mpango wa kuwakutanisha na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ili watembezwe kwenye vivutio na wavitangaze," alisema Mwaselela.

Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, ambaye alikutanishwa na warembo hao, aliiomba serikali na wadau mbalimbali kuwawezesha kiuchumi mabinti hao ili wafikie malengo ya maisha yao.

Alisema kwa umri wa vijana hao ambao baadhi yao ni wasomi lazima wana ndoto ambazo wanahitaji kuzifikia, lakini wanashindwa kwa sababu ya tatizo la kiuchumi na hivyo wakiwezeshwa wanaweza wakatimiza ikiwamo kuanzisha biashara na hata kufungua viwanda.

"Ni kweli wameshinda kwenye michujo waliyopitia kwenye mikoa yao, sasa baada ya kupatikana wanawezeshwaje? Ni vizuri ukawekwa utaratibu wa kuwawezesha ndoto zao zitimie," alisema Dk. Tulia.

Alimpongeza Mwaselela kwa kuwawezesha warembo hao kufika mkoani humo, huku akiwataka kwenda kuwa mabalozi wa vitu vizuri walivyoviona Mbeya.





# Maalim Seif ateuliwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amemteua Maalim Seif Sharif Hamad kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar na kukamilisha muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, kwa mujibu wa katiba.

Maalim Seif anachukua nafasi hiyo kwa mara ya pili, ambapo kwa mara ya kwanza mwaka 2010/2015 alichukua nafasi hiyo, baada ya kupata asilimia 49.14 ya kura katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2010 na mgombea wa CCM, Dk. Ali Mohamed Shein kupata asilimia 50.11.

Wakati huo Maalim Seif alikuwa mgombea urais wa Zanzibar kupitia CUF ambapo kwa mara ya kwanza Zanzibar ilianza na muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Kwa mujibu wa matokeo ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, Chama cha ACT -Wazalendo kina viti vya majimbo manne kwa nafasi ya uwakilishi, lakini kiti kimoja kipo wazi baada ya Mwakilishi Mteule wa Jimbo la Pandani, Abubakar Khamis Bakari, kufariki dunia kabla ya kula kiapo.

Ili kukamilisha muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, Rais Dk. Mwinyi pia anatarajia kujaza nafasi za wizara mbili ambazo aliziacha wazi wakati alipounda Baraza la Mawaziri.

Wakati akitangaza Baraza la Mawaziri, Dk. Mwinyi alisema ametenga nafasi mbili ambayo ni Wizara ya Biashara na Viwanda, na Wizara ya Afya Maendeleo na Jinsia kwa chama cha upinzani ambapo kimefikisha masharti ya katiba ya Zanzibar ya kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa mgombea anayepata zaidi ya asilimia 10 ya kura za urais.

Kwa mujibu wa taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa juzi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Dk. Abdulhamid Yahya Mzee, uteuzi huo wa Maalim Seif umeanza Juzi Desemba, 6,2020.

Aidha, taarifa hiyo ilieleza kwamba kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 9(3) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, kinachosema kwamba: "Muundo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar utakuwa wa Umoja wa Kitaifa na utendaji wa kazi zake utafanywa katika utaratibu utakaohakikisha kuendelezwa kwa umoja nchini na lengo la kufikia demokrasia."

Hatua hiyo imekuja baada ya Chama cha Upinzani cha ACT-Wazalendo kuafika uamuzi wa kujiunga na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Awamu ya Nane itakayokuwa na muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, akizungumza na waandishi wa habari juzi, alisema kuwa katika mkutano maalum wa kamati kuu ya chama hicho wameamua kupendekeza jina la mwanachama atakayekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar.

Sambamba na hayo, chama hicho pia, kimeruhusu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, wabunge, na madiwani waliochaguliwa kukiwakilisha chama hicho na wananchi waliowachagua kushiriki kikamilifu katika nafasi zao walizochaguliwa.

Mwafaka uliozaa maridhiano ya serikali ya umoja wa kitaifa ulitokana na mpasuko wa kisiasa uliojitokeza mwaka 2001 baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2000 na kusababisha zaidi ya watu 30 kupoteza maisha katika maandamano yaliyoitishwa na CUF kupinga matokeo ya uchaguzi mkuu na matukio yaliokuwa yamejitokeza.



Programu Meneja Elimu na Vijana (VSO), Bonavita Eahaihi (katikati), akiwashauri watendaji wa Green House kuzalisha bidhaa zenye ubora, Fuoni Kibondeni Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# SMZ yavutiwa ushiriki wa NMB katika uchumi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

VIONGOZI wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na chama tawala wamevutiwa na jinsi Benki ya NMB ilivyojipanga kushiriki katika shughuli za maendeleo visiwani humo na mchango inaoutoa kujenga uchumi imara wa kisasa.

Wakizungumza wakati wa hafla ya Usiku wa Taarab Zanzibar, Jumamosi, viongozi hao waliipongeza Benki ya NMB kufanya kazi karibu na serikali, huku wakiahidi ushirikiano wa kutosha na benki hiyo.

NMB inashiriki kuijenga Zanzibar kupitia huduma zake mbalimbali na imejipanga kushirikiana na Serikali ya Dk. Hussein Ali Mwinyi kutekeleza miradi mbalimbali.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna, alisema benki hiyo si tu kuwa ina nia ya kusaidia maendeleo ya Zanzibar, lakini ina msuli wa kuchangia kifedha.

"Benki ya NMB ina uwezo mkubwa kushiriki katika miradi mikubwa ya kimkakati. Benki ina mezania ya zaidi ya trilioni 7 sasa, mtaji na ukwasi wa kutosha," Zaipuna alifafanua na kuongeza kuwa NMB ni benki ambayo ina uwezo na iko tayari kushiriki katika miradi mikubwa ya kimkakati.

Zaipuna aliongeza: "Mheshimiwa Rais, tumejipanga vyema kuwahudumia wananchi wa visiwani na kusaidia kutimiza maono ya serikali mpya."

Kuhusu uchumi huo, Zaipuna alisema: Benki ya NMB imejipanga kushirikiana na serikali kutimiza maono yake kwenye uchumi wa bluu na tayari tumeanza kwa vitendo. Wiki hii tumetoa elimu ya kuwajengea uwezo wavuvi, wakulima wa mwani na wavunaji wa chumvi.

# Wamachinga Darajani kuunda kamati kuhamia Kibandamaiti

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa Mjini Magharibi Unguja, Idrissa Kitwana Mustafa, amewaagiza wafanyabiashara wadogo wa eneo la Darajani kuunda kamati ya watu watano itakayowawakilisha katika mazungumzo ya matayarisho ya kuhamia katika eneo la Kibandamaiti.

Kitwana alisema hayo wakati akizungumza na wafanyabiashara wa eneo la Darajani ambalo kwa sasa serikali inataka kufanya matengenezo na kuliimarisha eneo hilo.

Alisema kwa sasa wafanyabiashara hao wanatakiwa kubaki katika eneo la Kijangwani ambalo waliwekwa kwa muda huku eneo la Kibandamaiti likiwa linapangwa na kufanyiwa matengenezo kwa ajili ya wafanyabiashara ili kupisha shughuli za kufanyia matengenezo eneo la Darajani.

"Nawaomba sana mjichagulie viongozi wenu watano ambao tutafanya nao mazungumzo katika kulipatia ufumbuzi suala hili kwa vile serikali inataka kuliimarisha eneo hili, lakini na nyinyi tuwatengenezee mazingira mazuri ya kufanya shughuli zenu," alisema.

Aidha, alisema serikali imedhamiria kuimarisha shughuli za kiuchumi pamoja na kuwajengea mazingira bora wafanyabiashara wadogo ili kijikimu kimaisha.

"Rais Dk. Mwinyi anawapenda sana wananchi wake, amedhamiria kuleta mageuzi makubwa ya kiuchumi, hivyo kwa unyenyekevu mkubwa...tunaomba mtii maagizo haya ya serikali ya kuhama eneo hili kwa amani kabisa tukatafute riziki zetu, huku tukianza na maandalizi ya upangaji wa mji wetu," alisema Kitwana.

Hata hivyo, alisema serikali ya mkoa huo itaendelea kuwashirikisha wafanyabiashara hao kwa kila hatua ya mipango ya shughuli zao na kuwafuatilia kwa karibu ili kufanyakazi zao bila ya changamoto.

Akizungumzia suala la kulipa kodi, Kitwana alisema kodi ipo kisheria, hivyo aliwataka wananchi na wafanyabiashara katika mkoa huo, kulipa kodi ili kuongeza kasi ya maendeleo na kuinua uchumi wa nchi.

Kwa upande wao wafanyabiashara hao waliiomba serikali kuwapangia maeneo maalum ya kufanyia biashara zao katika eneo la Darajani kwani eneo hilo ndio lenye harakati nyingi za kibiashara kutokana na wingi na mahitaji ya watu.

"Waheshimiwa sisi sio kama tunakataa maagizo na maelekezo ya serikali, lakini tunaomba mtupangie maeneo maalum na mturuhusu kufanya biashara hapa Darajani kwani ndipo penye harakati na shughuli za watu," alisema Ali Khamis, mfanyabiashara wa eneo hilo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL**

Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile:

- **Kuboresha biashara**
- **Kulipa kodi ya nyumba**
- **Kumalizia tenda**
- **Kulipa matibabu n.k.**

Mawasiliano yetu:
**Dar es salaam – 0768 928 516.**
**Arusha – 0677 226 960.**

## NAFASI ZA KAZI

**Nafasi za kazi ya ualimu Diploma**
**- Kiswahili**
**-Science SST**
**- Kiingereza**
**Mawasiliano:**
**0783 334653**

NIPASHE NI JIBU LAKO
NJOO UTANGAZE NASI
KWA BEI NAFUU SANA
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**

Usimamizi wa mirathi No;365/2020
Ombi la BENEZETH MUGYABUSO MUTAYOBA,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu SALOME KOKUSHUBILA MUTAYOBA.Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 28/01/2021 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 02/12/2020.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**

Usimamizi wa mirathi **No;368/2020** Ombi la **IBRAHIM MKUDE HASSAN,**Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **MKUDE HASSANI HADILONGA.**Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe **14/12/2020** kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe **03/12/2020.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**JOVINUS LUGAIGANISA** AMEPOTELEWA NA VYETI,CHA KIDATO CHA NNE CHENYE **INDEX NAMBA S 2524-0023** KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI KUPITIA SHULE YA SECONDARY MURUSAGAMBA MWAKA **2009,CERTIFICATE** OF IT DIPLOMA YA CHUO CHA KAMPALA INTERNATIONAL **NAMBA CIT/3835/303/DT,CHETI** CHA DIPLOMA **NAMBA DCS/7089/401/DIT,** YEYOTE ATAKAYEVIOKOTA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI
**POLISI TAARIFA**
**DAR/STA/RB/825183/2020**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**ROSE SHEM MAYANI** anatangaza kupotelewa kwa result slip ya kidato cha nne yenye **index namba S.5429/0025** iliyotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya sekondary **TWING MEMORIAL** mwaka **2019** pamoja na leaving certificate ,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**Polisi taarifa**
**DAR/GOG/RB/802956/2020**

## General Company Limited

### TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**MUJUNI BWEKEA.....................MDAI**

**DHIDI YA**

**CRJE (EAST AFRICA) LIMITED.............MDAIWA**

Kwa mamlaka tuliyopewa na Mahakama Kuu ya Tanzania, MWANZA, tutauza mali kama ifuatavyo:-

| AINA YA MALI | NAMBA ZA USAJILI | TAREHE YA MNADA | ENEO LA TUKIO |
|---|---|---|---|
| Mitsubishi (FUSO) | T 590 BSD | 10/12/2020 | BUSWELU-MWANZA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mshindi atatakiwa kulipa pesa zote 100% eneo la tukio
2. Mali itauzwa jinsi ilivyo.

**Kwa mawasiliano Zaidi:-**
**0655 745071 & 0621 745071.**

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI
INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM.
MOB:
+255 - 0782253676

OFISI ZA MATANGAZO
Mikocheni Industial Area,
Po.Box 31042, Dar es Salaam.
Mob: +255 - 745 700 710.
E-mail:advertise@guardian.co.tz,
website: www.ippmedia.com

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Rais Tshisekedi avunja serikali ya muungano

**Kinshasa, DRC**

RAIS wa Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo (DRC), Félix Tshisekedi, ameamua kuweka mpango wa kuvunja serikali ya muungano na wafuasi wa aliyekuwa rais wa taifa hilo, Joseph Kabila.

Katika hotuba yake kupitia matangazo ya televisheni Jumapili, Tshisekedi alisema atachagua maofisa wapya kuunda baraza jipya kwa kuwa bunge la sasa lina wafuasi wengi wa Kabila, ambao hawamsikilizi.

Alisema alikuwa amejiandaa kuvunja bunge lote kama kuna ulazima.

Takribani miaka miwili sasa, DRC iliunda serikali ya muungano, baina ya chama cha Kabila na chama cha rais mpya Tshisekedi, vyama viwili ambavyo vilipingana kwa kipindi cha muda mrefu vilikubaliana kufanya kazi kwa pamoja, lakini baada ya siku chache tu, mvutano ulianza kati ya vyama hivyo.

Baadhi ya wafuasi wa Chama cha Tshisekedi walianza kususia ushirikiano huo, huku wakiwashutumu wafuasi wa chama cha Kabila kumzuia rais mpya kutekeleza ahadi zake.

Hivi karibuni, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN) na kiongozi wa Umoja wa Afrika (AU) walieleza wasiwasi wao juu ya mvutano wa kisiasa wa pande zote mbili.

***BBC***



Magari ya zimamoto yakiwa kwenye ufukwe wa kisiwa cha Fraser Island wakati mamlaka zikitumia ndege kukabiliana na moto ulioteketeza mita 700 za eneo la mji huo mdogo wa nchini Australia. **PICHA/BBC**

# UNHCR yakataa kuhamishwa kwa wakimbizi wa Rohingya

**Dhaka, BANGLADESH**

SHIRIKA la kuhudumia Wakimbizi la Umoja wa Mataifa (UNHCR), limesema linapinga kuhamishwa kwa wakimbizi wa Rohingya kutoka Cox Bazar, Bangladesh, kwenda kisiwa cha mbali katika Ghuba ya Bengal.

Mamlaka nchini Bangladesh, mwishoni mwa wiki, ilihamisha zaidi ya wakimbizi 1,500 wa Rohingya kwenda Bhasan Char, ghuba isiyo na wakazi wa kisiwa cha Bengal inayoweza kuathiriwa na vimbunga na mafuriko.

Msemaji Mkuu wa Ofisi ya Wakimbizi ya Umoja wa Mataifa, Babar Baloch, alisema Umoja wa Mataifa (UN), haukuhusika katika kuandaa harakati hiyo.

Alisema hakujua ni wakimbizi gani na alikuwa na habari chache sana juu ya operesheni ya jumla ya uhamishaji.

Alieleza UNHCR ina wasiwasi kuwa wakimbizi wa Rohingya hawakuwa na taarifa waliyohitaji kufanya uamuzi huru na ulio na taarifa kamili juu ya kuhamia Bhasan Char.

"Tumesikia ripoti kutoka kwenye kambi kwamba baadhi ya wakimbizi wanaweza kuhisi wanashinikizwa kuhamia Bhasan Char au labda wamebadilisha maoni yao ya mwanzo juu ya kuhamishwa na hawataki tena kuhama.

Ikiwa ni hivyo, wanapaswa kuruhusiwa kubaki katika kambi hizo," alisema Baloch.

Mwaka 2017, karibu wakimbizi milioni moja walitoroka mateso na vurugu huko Myanmar na kwenda Cox's Bazar ambako wanaishi katika kambi duni zenye msongamano wa watu.

Bangladesh inasema inataka kupunguza msongamano katika kambi hizo na inaona kuwahamisha hivi karibuni wakimbizi hao ni hatua ya kwanza katika mpango wa kuhamisha wakimbizi 100,000 kwenda Bhasan Char.

UN, ilitoa wito kwa serikali kuheshimu nia yake ya dhati kwamba harakati za kwenda katika kisiwa hicho, zitakuwa ni za hiari.

Baloch alisema UNHCR inasikitishwa na picha za wakimbizi walio na matatizo wakati wa mchakato wa kuhama na imepeleka wasiwasi wake kwa mamlaka za Bangladesh.

"Tunasisitiza tena kwamba harakati zote za kuhama kama ilivyotajwa hapo awali kwa Bhasan Char, lazima ziwe za hiari na kulingana na mashauriano na habari kamili juu ya hali ya maisha katika kisiwa hicho na haki na huduma ambazo wakimbizi wataweza kupata," aliongeza Baloch.

***VOA***

# Idadi ya vifo vya raia yaongezeka Yemen

**Sana'a, YEMEN**

RAIA wameendelea kupoteza maisha kwenye vita vya ndani vinavyoongezeka kila siku, nchini Yemen.

Ofisi ya Uratibu wa Masuala ya Kibinadamu ya Umoja wa Mataifa (UN) ilitangaza kuwa raia 139 waliuawa na kujeruhiwa katika miezi miwili iliyopita katika eneo la Hudayda kutokana mizozo iliyoongezeka.

Katika taarifa iliyotolewa na ofisi hiyo, ilisisitizwa kuwa pande zote zinazozozana zinapaswa kuacha mashambulizi dhidi ya raia, ambayo yanakiuka sheria za kimataifa.

Hadi kufikia sasa tangu kuanza kwa vita vya ndani vya Yemen, raia 12,000, na jumla ya watu 112,000 wamepoteza maisha.

Miongoni mwa watu waliopoteza maisha watoto ni 2,138.

Wakati huo huo, kamanda mwandamizi kutoka Baraza la Mpito la Kusini aliyekuwa akiungwa mkono na serikali ya Abu Dhabi, aliuawa katika mji wa Ebyen.

**TRT**

# Marekani, China zadhibiti soko la silaha

**Washington, MAREKANI**

RIPOTI mpya ya taasisi ya kimataifa ya utafiti wa amani (SIPRI), yenye makao yake mjini Stockholm, imeonyesha kuwa kampuni za silaha za China na Marekani zililidhibiti soko la silaha duniani kwa mwaka 2019.

Pia ripoti hiyo ilisema Mashariki ya Kati kwa mara ya kwanza imeingia kwenye orodha ya wazalishaji wakubwa zaidi 25 wa silaha.

Kulingana na takwimu zilizochapishwa na SIPRI jana, zimeonyesha kampuni za silaha ziliyojikita nchini Marekani zilichukua nafasi tano za mwanzo mwaka jana, wakati kampuni ya Lockheed Martin, Boeing, Northrop Grumman, Raytheon na General Dynamics zikifanya biashara ya dola bilioni 166 katika mauzo jumla ya mwaka.

Kwa ujumla, kampuni 12 za Marekani zimekuwa miongoni mwa kampuni 25 kubwa zaidi zinazozalisha silaha na kufanya asilimia 61 ya mauzo jumla ya silaha.

Aidha, kwa mara ya kwanza kampuni ya Ufaransa ya Dassault Aviation Group nayo imeingia kwenye orodha hiyo ya kampuni 25 kubwa za uzalishaji silaha.

Kampuni hiyo ilichangia ongezeko kubwa katika mauzo ya silaha ya kila mwaka kwa asilimia 105.

Kwa pamoja, mauzo ya silaha na huduma za kijeshi za kampuni hizo 25 zilifanya kiasi cha dola bilioni 361 kwa mwaka 2019, ambacho ni ongezeko la asilimia 8.5 tofauti na mwaka 2018.

**DW**

## HABARI MICHEZO

# VIGOGO SITA ENGLAND VYAMWANIA DYBALA




**LONDON, England**

PAULO Dybala anaweza kujipanga kuondoka kule Juventus - wakati nyota huyo akitajwa kuwaniwa na klabu kubwa sita za Ligi Kuu ya England.

Wawakilishi wa Dybala wamewasiliana na klabu hizo kubwa za England katika kuhakikisha uhamisho wa nyota huyo unafanikiwa kutoka Juventus mwakani, kwa mujibu wa tovuti ya 90min.

Dybala mkataba wake wa sasa na mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, unamalizika mwaka 2022, lakini aliripotiwa kwamba anakaribia kusani mkataba mpya.

Hata hivyo, Ligi Kuu ya England inaweza kuwa ndio kituo chake kinachofuata kwa raia huo wa Argentina mwenye umri wa miaka 27.

Klabu kubwa zinazotajwa kuwania saini yake ni Liverpool, Manchester City, Manchester United, Chelsea, Tottenham na Arsenal.

Dybala amecheza mechi 10 kwenye mashindano yote msimu huu kwa kikosi cha Juve, huku akifunga mara moja.



# PIOLI AKUNWA MILAN KUSHINDA BILA IBRAHIMOVIC

**MILAN, Italia**

STEFANO Pioli amesifia kukua na kupevuka kwa wachezaji wake wa AC Milan wakati wa kukosekana kwa straika, Zlatan Ibrahimovic ambaye ni majeruhi.

Rossoneri walijiimarisha kileleni mwa msimamo wa Serie A, wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Sampdoria Jumapili, shukrani kwa mabao ya Franck Kessie na Samu Castillejo.

Milan walipata ushindi huo bila ya nyota wao Ibrahimovic, ambaye anauguza majeruhi ya misuli, lakini anatarajia kurudi uwanjani haraka.

Mkongwe huyo wa kimataifa wa Sweden amefunga mabao 10 katika mechi sita za Serie A msimu huu, na alikosekana kwenye mchezo dhidi ya Sampdoria.

"Naendelea kushangazwa na kupevuka na kukua kwa wachezaji wangu," alisema Pioli akiiambia Sky Italia.

"Hata kama kilikuwa kikosi chenye wachezaji wengi vijana, walicheza vizuri. Hawakuwapa nafasi kabisa, kwa hakika walinivutia sana mimi.

"Wote tunajua kwa namna gani Zlatan alivyotusaidia sisi kuimarika na kila mmoja anataka arudi uwanjani haraka inavyowezekana, lakini kila mchezaji ana mchango wake hapa."

Milan imeshinda mechi nane kati ya 10 za Serie A na wanaongoza kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo kwa tofauti ya pointi tano dhidi ya Inter Milan.

# MOURINHO AMWAGA SIFA KWA HOJBJERG

**LONDON, England**

JOSE Mourinho amemtaja Pierre-Emile Hojbjerg kama "mchezaji wa aina yake" baada ya Tottenham Hotspur kupata ushindi kwenye mchezo wa 'dabi' ya Jiji la London dhidi ya Arsenal, Jumapili.

Son Heung-min na Harry Kane kila mmoja alifunga bao moja kuwawezesha Spurs kupata ushindi wa 2-0 kwenye Ligi Kuu England na kupaa kileleni mwa msimamo. Hojbjerg, alisajiliwa Agosti mwaka huu akitokea Southampton kwa ada iliyoripotiwa kuwa pauni milioni 15 na alikuwa muhimili mkuu wa ushindi huo.

Kiungo huyo aligusa mpira mara 61, pasi (44), pasi zilizofanikiwa (35), pasi zilizowapita wapinzani (15).

Hojbjerg mwenye umri wa miaka 25, akamwagiwa sifa kemkem na bosi wake huyo.



"Pierre kwanza ni mtu mwenye akili sana. Ndiye alikuwa kinara kwenye mchezo na ninaimani atakuwa kocha siku moja," Mourinho alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Kwa hakika kabisa, nimefurahishwa mno na kiwango chake, maana yeye ndiye alikuwa kiongozi wa mchezo wote.

"Dimbani anawaongoza wachezaji wote, alicheza vizuri na nina imani kubwa kwamba atakuwa msaada mkubwa kwa timu hii."

## HABARI MICHEZO




# KOEMAN

## AMPINGA RAIS KUUZWA MESSI

**BARCELONA, Hispania**

KOCHA wa Barcelona, Ronald Koeman amepingana na mawazo ya rais wa muda wa timu hiyo, Carlos Tusquets juu ya kuuzwa kwa Lionel Messi katika kipindi cha majira ya joto kilichopita.

Tusquets aliwaambia waandishi wa habari mapema wiki hii kwamba, Barcelona ilitakiwa imuuze Messi kwenye usajili wa msimu wa majira ya joto uliopita, kwani ingekuwa imetengeneza fedha kubwa kuliko kuondoka bure mwishoni mwa msimu huu.

Messi atakuwa nje ya mkataba mwishoni mwa msimu huu mara tu mkataba wake utakapomalizika.

Manchester City na Paris St-Germain ni miongoni mwa timu zinazowania saini yake.

"Binafsi sijali watu wa nje wanasema nini kuhusu sisi (Barca), lakini watu wa ndani wakiwa wanasema vibaya kuhusu timu inaondoa utulivu kambini na hili siwezi kukaa kimya hata kidogo," alisema Ronald Koeman kocha wa zamani wa Everton na Uholanzi.

Nyota huyo wa Argentina amekuwa ndani ya Nou Camp tangu mtoto na kwa asilimia kubwa ameitumikia taaluma yake pale Barca, na alishinikiza kuondoka Agosti ingawa ilishindikana kutokana na kile kilichosemwa kuwa ndani ya kipengele katika mkataba wake inahitajika timu kutoa pauni milioni 700.

## INFANTINO ATETEA MVUTO WA VAR

**NYON, Uswisi**



RAIS wa Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), Gianni Infantino amesema uwapo wa teknolojia ya usaidizi wa maamuzi kwa njia ya video kwa waamuzi wa soka (VAR), haujaharibu ladha ya soka na badala yake mfumo huo umeboresha.

Akizungumza na BBC Sport, rais huyo amesema amekuwa akifuatilia kwa karibu mchango wa VAR, ambapo amebaini kuwa kuna faida nyingi.

Wakati akisema hayo, nahodha wa Liverpool, Jordan Henderson na wa Aston Villa, Jack Grealish hivi karibuni walisema kwamba VAR inatakiwa iondolewe kufuatia maamuzi yaliyotafsiriwa kama ya uonevu dhidi yao.

"Inatakiwa tukumbuke tulianzisha mfumo huu miaka miwili tu iliyopita, na si miaka 20, alisema Infantino.

"VAR imesaidia mpira, nadhani imekuza mpira".

"Bodi ya Kusimamia sheria za soka duniani - FAB ambayo inasimamia matumizi ya VAR ina uhakika kuwa itafanya kazi bila shida.

"VAR imewasaidia waamuzi kwenye Kombe la Dunia, imewasaidia waamuzi kwenye kila mashindano, wachezaji na makocha," aliongeza kusema Infantino.



## KLOPP ATUMAINI WIJNALDUM ATASAINI MKATABA MPYA

**LIVERPOOL, England**

JURGEN Klopp ana matumaini kwamba, Georginio Wijnaldum atasaini mkataba mpya na Liverpool.

Raia huyo wa Uholanzi yupo kwenye mwaka wake wa mwisho katika mkataba wake aliousaini mwaka 2016 wakati alipotua hapo akitokea Newcastle United na Januari atakuwa uhuru kuzungumza na klabu yoyote.

Barcelona wametajwa mara kwa mara kwamba wanahitaji saini yake, kwani kocha wao wa sasa, Ronald Koeman ameshafanya kazi na Wijnaldum kwenye kikosi cha timu ya Taifa ya Uholanzi.

Hata hivyo, baada ya kumuona nyota huyo wa zamani wa PSV akifunga wakati Liverpool wakiibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Wolves Jumapili, Klopp alibainisha kwamba hajakata tamaa kwa mchezaji huyo kubaki hapo kwenye dimba la Anfield.

Alipoulizwa kuhusu uwezekano huo, raia huyo wa Ujerumani aliiambia Amazon Prime Sport: "Nina matumaini hayo, kiukweli kabisa.

"Unaweza kuona kwamba anacheza wakati wote, anacheza kwa muda mrefu dimbani na nimekuwa na mahusiano naye mazuri. Nina matumaini atabaki."

Wijnaldum amefunga mabao 26 kwenye Ligi Kuu kwa ujumla wake tangu ahamie Newcastle mwaka 2015.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# ARTETA ATUPIA ZIGO MASTRAIKA ARSENAL

●●● Nilishasema tunawahitaji washambuliaji wetu kufunga, tunahitaji mabao yao, lakini mambo...

**LONDON, England**

MIKEL Arteta amewalaumu mastraika wake kwa kushindwa kufunga wakati Arsenal ikichezea kichapo cha 'dabi' ya London Kaskazini kutoka kwa Tottenham Hotspur, kwenye Ligi Kuu ya England juzi.

Mabao kutoka kwa Son Heung-min na Harry Kane yalikipa kikosi cha Jose Mourinho ushindi wa 2-0 Jumapili.

Pierre-Emerick Aubameyang alishindwa kabisa kupiga shuti hata moja golini, huku patina wake wa safu ya ushambuliaji, Alexandre Lacazette akipiga mawili tu.

Licha ya Arsenal kumiliki mpira kwa asilimia kubwa ya 69.2 dhidi ya 30.8 ya Tottenham na kupiga krosi nyingi zaidi za wazi (32) tangu Februari 2016, lakini haikuweza kupata matokeo chanya.

Umekuwa msimu mgumu kwa Aubameyang na Lacazette, ambao kwa pamoja wamehusika katika mabao matano tu kwenye Ligi Kuu.

Lakini ukiwalinganisha wao na Kane na Son wana mabao 18 na pasi za mwisho 13 kwa pamoja na wote walifunga kwenye mchezo huo wa juzi.

"Ukiangalia kwa takwimu zote, mchezo tuliumiliki sisi, lakini mwisho wa siku ni suala la kuuweka mpira nyavuni," alisema Arteta akiviambia vyombo vya habari baada ya mchezo huo.

"Tulikuwa na nafasi. Pengine tulitengeneza nyingi zaidi kwa msimu huu, lakini kuutupia mpira wavuni lilikuwa jambo gumu kwetu.

"Lakini mwisho wa siku tulitakiwa kufunga mabao na wao walipata nafasi wakafunga na sisi tulishindwa.

"Tuhahitaji kujenga kitu fulani, tunahitaji matokea chanya tu.

"Nimejaribu kila namna kuangalia tucheze vizuri, lakini naona natumia nguvu na mastaa wetu hawaonyeshi kubadilika katika kila mchezo tunaokuwa uwanjani.

"Nilishasema, tunawahitaji washambuliaji wetu kufunga, tunahitaji mabao yao ili tuweze kuwa na matokeo mazuri, lakini mambo yamekuwa tofauti kabisa.

"Mwisho wa siku huu ni mchezo wa soka na tunachotakiwa kupata ni ushindi tu, lakini tumepoteza tena leo (juzi)."

Wakati alipoulizwa namna gani Arsenal, ambao kwa sasa wapo nafasi ya 15 wakipitwa pointi 11 na vinara Spurs wanaweza kurudisha matokeo, Arteta alisema anaimani mambo yanaweza kubadilika.

"Kwa kufunga mabao, ni rahisi," alisema. "Tunahitaji kufunga mabao na hilo ndilo jambo pekee kwetu."

## KWA UFUPI

**RONALDO KUREJESHWA UNITED**

WADHAMNI wa jezi ya Manchester United, Chevrolet wanaamini litakuwa jambo la thamani kibiashara kusaidia kufadhili hatua ya kumrejesha, Old Trafford mshambuliaji wa Juventus na Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 35. ***(Auto Esporte, via Sun)***

**DYABALA LULU EPL**

MSHAMBULIAJI wa Juventus na Argentina, Paulo Dybala mwenye umri wa miaka 27, amepata ofa za timu kubwa sita za Ligi Kuu England, Manchester United, Liverpool, Chelsea, Tottenham, Manchester City na Arsenal. ***(90Min)***

**POGBA ASIMULIA CORONA**

KIUNGO wa Manchester United, Paul Pogba ambaye alikutwa na maambukizi ya virusi vya corona Agosti mwaka huu amesema alijikuta "anachoka haraka" baada ya kukimbia muda mchache kwenye mazoezi. ***(MUTV, via Mirror)***

**OZIL KUONDOKA ARSENAL**

KIUNGO wa Arsenal, Mesut Ozil mwenye umri wa miaka 32, anaamini kuwa ataweza kupata klabu nyingine bora, lakini ana uwezekano wa kuondoka kabla ya msimu ujao. ***(Mail)***

**TRIPPIER AWANIWA UNITED**

MANCHESTER United inamfuatilia mlinzi wa Atletico Madrid, Kieran Trippier mwenye umri wa miaka 30 raia wa England, huku Ole Gunnar Solskjaer akimhitaji kwa ajili ya kumpa changamoto, Aaron Wan-Bissaka mwenye miaka 23. ***(Telegraph)***

**WIJNALDUM AISUBIRI LIVERPOOL**

KIUNGO wa kati wa Liverpool, Georgio Wijnaldum mwenye umri wa miaka 30 raia wa Uholanzi, amedokeza kuwa anasubiri klabu ichukue hatua kuhusu kuongeza mkataba wake. ***(Mirror)***

**ARSENAL BADO KWA SZOBOSZLAI**

ARSENAL inaweza kulazimika kuharakisha uhamisho wa Dominik Szoboszlai wakati wa dirisha la Januari, baada ya habari kuibuka kuwa Real Madrid wamepanga kutoa kitita kirefu cha fedha kwa ajili ya nyota huyo wa kimataifa wa Hungary anayekipiga kule Salzburg. ***(Express)***

**PSG CHALI KWA MESSI**

MKURUGENZI wa michezo wa Paris St-Germain, Leonardo ameondoa matarajio ya klabu hiyo kumsajili nyota wa Barcelona na Argentina Lionel Messi kama mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, ataondoka Barcelona mwakani. ***(Mail)***

**WEST HAM YAMFUATA EDWARDS**

West Ham ni miongoni mwa klabu za England na Ureno zinazomtolea macho mchezaji wa zamani wa Tottenham Hotspur, Marcus Edwards ambaye ni winga wa kimataifa wa Uingereza mwenye umri wa miaka 22, kwa sasa akiichezea Vitoria Guimaraes. ***(Team Talk)***

**O'NEILL AMKATAA MCNAIR**

KOCHA wa Stoke City, Michael O'Neill amekanusha madai ya kutaka kumsajili mlinzi wa Middlesbrough na Ireland Kaskazini, Paddy McNair mwenye umri wa miaka 25, kipindi cha majira ya joto kijacho. ***(Teesside Gazette)***

**ALMADA HUYOOO UNITED**

KLABU YA Manchester United imeibuka kuwa kinara katika kinyang'anyiro cha kupata saini ya kiungo wa kati wa Argentina, Thiago Almada mwenye umri wa miaka 19 anayeichezea Velez Sarsfield. ***(Todo Fichajes, via Team Talk)***

## HABARI MICHEZO

# RUVU SHOOTING YATAJA 'USALITI' KIPIGO YANGA

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Kocha Mkuu wa Ruvu Shooting, Boniface Mkwasa, akikubali matokeo na kueleza uzoefu na uwezo wa mchezaji mmoja mmoja umewabeba wapinzani wao, Yanga kuibuka na ushindi, Ofisa Habari wa timu hiyo, Masau Mbwire amemtaja "Yuda" (kuwapo kwa 'usaliti') katika kipigo cha bao 1-0 walichokipata juzi.

Baada ya mechi hiyo, iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi, Mkwasa alikubali matokeo na kueleza kwamba amekuwa na wakati mgumu anapocheza na Yanga ama Simba kulingana na aina ya uchezaji wa timu hizo pamoja na wachezaji kujitoa na kujituma kuhakikisha wanapata matokeo katika mechi zao.

"Hakuna urahisi wa hizi timu mbili unapocheza nazo, kikubwa ni jisni maandalizi na jinsi ya mfumo ambao utaingia nao, nilifanikiwa kupata ushindi Simba kwa sababu wachezaji walikuwa makini kutumia nafasi tulizotengeneza, lakini dhidi ya Yanga walipoteza umakini," alisema Mkwasa.

Lakini kwa upande wa Masau Bwire, alisema kipigo walichokipata kinamkumbusha zamani enzi ya Yuda Iskarioti.

"Mchezo wa leo unanikumbusha enzi hizo. Unanikumbusha bwana mmoja anaitwa Yuda. Kwa wale wanaokumbuka maandiko, watamjua bwana Yuda ni nani na alifanya nini," alisema Masau ambaye aliongea kwa mifano zaidi na kwa tahadhari. Alisema kuwa vijana wa Ruvu Shooting walicheza kandanda safi, lakini kutokana na sababu hizo anazozisema, wameshindwa kupata ushindi.

"Naomba waandishi mfuatilie ili mjue Yuda ni nani na amefanya nini. Tulijiandaa, tulifanya maandalizi makubwa na tuliamini kuwa tutashinda, lakini kutokana na sababu niliyosema, Yanga wakapata ushindi kwa hali hiyo waliyoipata," alilalama Bwire.

Kwa mujibu wa maandiko, Yuda Iskarioti ni mmoja wa wanafunzi wa Yesu ambaye baadaye alimsaliti kwa Wayahudi kwa vipande vya fedha.

HONGERA...



Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Rais mstaafu Jakaya Kikwete (wa pili kulia), akimkabidhi zawadi, Ofisa Masoko wa Kampuni ya The Guardian Limited, Lameck Samson, baada ya kuibuka mshindi wa kwanza wa mbio za UDSM Marathon kwa upande wa watu wenye uhitaji maalum. Mbio hizo zilizofanyika mwishoni mwa wiki chuoni hapo, zilidhaminiwa na Benki ya Taifa ya Biashara, NBC. **MPIGAPICHA WETU**

# DStv yaongeza msisimko zaidi msimu wa sikukuu

**Na Mwandishi Wetu**

KUELEKEA msimu wa sikukuu hizi za mwisho wa mwaka, msisimko zaidi umeongezwa ndani ya DStv, ili kukufanya kuwa na nyakati nzuri zaidi za kusherehekea na familia yako vyovyote itakavyokuwa, imeelezwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mutlichoice Tanzania, Jacqueline Woiso, amesema tayari DStv imefurika misisimko na wingi wa maudhui kwenye msimu huu wa sikukuu, hivyo kila mmoja anakaribishwa kuungana na familia yake na marafiki ili afurahie sikukuu kwa vipindi na michezo inayofaa kwa wakati wowote.

"DStv inazingatia mahitaji ya wateja wake wote katika kila kitu tunachofanya ili kuhakikisha wateja wetu wanaunganishwa na maudhui bomba na kukidhi matarajio makubwa ya mteja.

"Ni kwa kuzingatia hilo ambapo chapa imezingatia mahitaji ya wateja, imeifikiria upya mioyo ya wateja kuonyesha uwapo wa chapa huku ikidhihirisha kweli hii ni chapa ya hapa nyumbani inayoboresha na kuhamasisha maudhui ya nyumbani," alisema Woiso na kuongeza;

"Tunataka kila mtu awe sehemu ya familia ya DStv msimu huu wa sikukuu na kusherehekea nyakati za kawaida pamoja. Msimu huu wa sikukuu unaweza kufurahia wakati wowote unaotaka kutoka kwenye upana wa maudhui ya nyumbani na kimataifa."

Alisema DStv inawaletea wateja wake nyakati za kufurahisha, wakiwa wameketi kwenye kiti, huku mapigo yao ya moyo yakienda mbio wakati wanapotazama Ligi Kuu England kupitia SuperSport.

"Pia tusisahau jinsi nyakati hizi za mapumziko zilivyo muhimu katika kutulia na familia ambapo babu, bibi na familia hupata wasaa mzuri na watoto kuangalia vipindi kama PJ Masks kwenye Disney Jr."

Alisema DStv inajua fahari uliyonayo unapotazama maudhui ya nyumbani, hivyo inaongeza nyakati hizo za kujivunia kwenye safu yako na vipindi vya nyumbani kama vile, Karma, Slay Queen, Kitimtim na vingine vingi kwenye Maisha Magic Bongo.

"Tazama vipindi hivi ukiwa na familia na marafiki, hata majirani zako ili uufanye utazamaji wako wa furaha katika msimu huu wa sikukuu," alisisitiza.

## Askari JWTZ ashikiliwa tuhuma kumpiga refa

**Na Rose Jacob, MWANZA**

JESHI la Polisi Mkoa wa Mwanza, linamshikilia Askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Silvanus Silvester (37), kwa tuhuma za kumshambulia kwa mateke na kichwa mwamuzi wa mchezo wa mpira wa miguu kati ya timu ya Pamba na Rhino Rangers, Fadhili Mwaka, uliopigwa katika Uwanja wa Nyamagana wiki iliyopita.

Kamanda wa Polisi, Mkoa wa Mwanza, Muliro Jumanne, alisema askari huyo wa JWTZ mwenye namba MT.85507 CPL, kuwa mbali na tuhuma hizo za kumshambulia mwamuzi huyo, pia anadaiwa kuharibu kamera ya mwandishi wa habari uwanjani hapo.

Kamanda Muliro aliitaja kamera iliyoharibiwa kuwa ni aina ya Canon mali ya mwandishi Abdarah Chausiku na kwamba askari huyo alitenda kosa hilo Desemba 5, mwaka huu majira ya saa 10:50 alasiri katika mechi hiyo ambayo ilikuwa ya Ligi Daraja la Kwanza.

Alisema mtuhumiwa huyo anatarajiwa kufikikishwa mahakamani baada ya upelelezi kukamilika.

## Banda ataja siku kurejea dimbani

**Na Saada Akida**

BAADA ya kutoonekana uwanjani kwa muda mrefu, beki wa zamani wa Simba, Abdi Banda, ambaye anaichezea Klabu ya Highlands Park ya Afrika Kusini, amevunja ukimya kwa kueleza kwamba majeraha ya paja ndiyo yamemfanya kuwa nje ya dimba kwa takriban miezi mitano sasa akipata matibabu.

Banda aliliambia Nipashe kuwa alipata majeraha hayo tangu Agosti mwaka huu na alitakiwa kuwa nje ya uwanja kwa miezi mitano akijiuguza.

"Ukiachilia kila mtu kuongea lake na kuleta sintofahamu na mimi kukaa kimya muda mrefu bila kujibu chochote, ukweli ni kwamba niko katika matibabu na sasa naendelea na mazoezi madogo madogo chini ya uangalizi wa daktari Chans-Simz na wasaidizi wake," alisema Banda.

Alisema kutokana na matibabu anayoendelea kuyapata huku akiendelea na mazoezi, anatarajia hadi Januari mwakani anaweza kurejea uwanjani kuendelea na majukumu yake.

Banda ambaye kabla ya kutua Simba na kuitumikia kuanzia mwaka 2014-2017, aliichezea Coastal Union ya Tanga na wakati akitokea kwa 'Wekundu wa Msimbazi' hao, alitua moja kwa moja Baroka FC ya Afrika Kusini na kuitumikia kuanzia mwaka 2017-2019 na kisha kujiunga na Highlands Park.

Michezo
Jumanne Desemba 8, 2020
Nipashe



ARTETA ATUPIA ZIGO MASTRAIKA ARSENAL HABARI UK 22

CHA KWANZA...



Mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah (Kulia), akiifungia timu yake bao la kwanza dhidi ya Wolves wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 4-0 kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Anfield juzi. Mabao mengine yalifungwa na Georginio Wijnaldum, Joel Matip na Nelson Semedo. **PICHA: MTANDAO**

# SARPONG AMWAMSHA KAZE MABAO YANGA

Aeleza anavyomfukuzia Bocco kimya kimya, akunwa na mabadiliko akimtaka kutumia...

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, amesema ameona mabadiliko kidogo katika safu yake ya ushambuliaji na kumtaka mshambuliaji wa timu hiyo, Mghana Michael Sarpong, kuendeleza kasi yake ya kupambana kuhakikisha anaendeleza spidi ya kufunga kila anapompa nafasi ya kucheza.

Hatua hiyo imekuja baada ya Yanga kuibuka na ushindi wa 2-1 dhidi ya Ruvu Shooting, huku Sarpong akifunga la kwanza dakika ya 30 na kufikisha mabao manne kwenye Ligi Kuu hadi sasa, wakati huu mshambuliaji wa Simba, John Bocco akiwa kileleni mwa orodha ya wafungaji wa ligi hiyo kutokana na kucheka na nyavu mara saba.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kaze alisema kufunga kwa Sarpong katika mchezo dhidi ya Ruvu Shooting bado hawezi kuweka wazi kwamba safu yake ya ushambuliaji iko vizuri, hivyo anamtaka kupambana zaidi, huku akiongeza umakini na utulivu anapokuwa uwanjani.

Alisema ilikuwa mechi ngumu kutokana na timu waliyocheza nayo kufundishwa na kocha mzoefu, lakini tatizo kikosi chake kimekuwa kikitengeneza nafasi nyingi na kushindwa kuzitumia.

"Sarpong amefunga leo, amefikisha mabao matano [manne] hayupo mbali na anayeongoza katika ufungaji ambaye ana mabao saba, lakini sitahesabu kwamba safu ya ushambuliaji imekuwa na mabadiliko makubwa bali anapaswa kuendelea kufunga kila mechi," alisema Kaze.

Alisema anaendelea kuwasisitizia washambuliaji wake kuwa watulivu wanapokuwa uwanjani, ambapo tayari amefanikiwa katika nafasi zingine ikiwamo ya ulinzi, viungo pamoja na mawinga ambao walifanya kazi nzuri katika michezo mitatu iliyopita.

"Wachezaji wangu wanafuata maelekezo ndani ya uwanja jambo linalowafanya wanapata matokeo chanya, lakini kutumia vema makosa wa wapinzani kuwa faida kwetu," alisema Kaze.

Alisema hatua ya kumuita Deus Kaseke baada ya kukosa mkwaju wa penalti, lengo kubwa lilikuwa kumtuliza na kumtaka asahau makosa hayo.

Kuhusu ujio wa Saidi Ntibazonkiza, alisema ni mchezaji mzuri na atakuwa msaada mkubwa ndani ya kikosi cha timu hiyo kwa sababu anafahamu uwezo wake pamoja na uzoefu alionao katika soka.

"Ni mchezaji mzuri, ana uzoefu mkubwa kwa sababu amecheza soka Ulaya muda mrefu, ataongeza nguvu na uzoefu aliokuwa nao kwa wachezaji ambao wapo hapa, suala la ufungaji nina imani bado nitaendelea kuwapa mbinu mpya ili tutoke katika kupata bao 1-0," alisema kocha huyo.

Kaze akisaidiwa na mzawa, Juma Mwambusi wameiwezesha Yanga kuendeleza rekodi yake ya kutopoteza mchezo wowote hadi sasa tangu aipokee kutoka kwa Mserbia Zlatko Krmpotic, ambapo sasa ipo kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 34 zilizotokana na mechi 14.

## AZAM YAIACHIA SIMBA KUIPIKU

**Na Adam Fungamwango**

BADO inaonekana Azam FC pumzi yake ya kuwafukuza vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara Yanga ni ndogo, baada ya jana kulazimishwa suluhu dhidi ya Gwambina FC na kuwaacha wakitanua kileleni bila presha kubwa, huku ikizidi kufungua njia kwa Simba kuipiku endapo itashinda viporo vyake.

Sare ya bila kufungana ambayo Azam imetoka kwenye Uwanja wa Gwambina jana, imeifanya timu hiyo kuongeza pointi moja tu na kufikisha 27, pointi saba nyuma ya vinata Yanga baada ya timu hizo kila moja kushuka dimbani mara 14 hadi sasa.

Matokeo hayo yanaifanya Simba ambayo ina pointi 23 baada ya kushuka dimbani mara 11, kuhitaji alama tano tu katika michezo yake mitatu ili kuishusha Azam hadi nafasi ya tatu ya msimamo wa ligi hiyo, lakini kama itashinda zote itakuwa nyuma ya Yanga kwa pointi mbili.

Haikuwa mechi rahisi kwa Azam, kwani ilikutana na wakati mgumu kwa kushambuliwa karibuni muda wote wa mchezo, huku yenyewe ikifanya mashambulizi machache ambayo mengi hayakuwa ya hatari.

Ilikuwa ni dakika ya 36 wakati mshambuliaji hatari wa Gwambina FC mwenye magoli sita mpaka sasa, Meshack Abraham, alipoachia shuti kali akiwa kwenye winga ya kushoto, lakini lilitoka sentimeta chache kwenye goli la Azam.

Kipa wa Azam aliyekuwa benchi muda mrefu, Benjamin Haule jana alikuwa nyota wa mchezo kwa kuokoa hatari nyingi, kwani dakika ya 54 alipangua mkwaju wa faulo uliopigwa na Rajab Athumani na kuwa kona ambayo haikuzaa matunda.

Jimson Mwanuke, ndiye mchezaji wa Gwambina ambaye itabidi ajilaumu mwenyewe kwa kukosa mabao mengi, mojawapo likiwa dakika ya 59, alipowazidi mbio mabeki wa Azam na kuachia shuti kali lililopaa kidogo juu la lango la Azam ambayo ilikuwa ikiongozwa na Kocha Msaidizi Vivier Bahati, kutokana na kocha mpya, George Lwandamina akiwa anashuhudia benchini.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002